# Nipashe

Jumatano Desemba 2, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580417

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**NBS** yaokoa bil. 2/- sensa ya mifugo, uvuvi, kilimo

UKURASA 8




**Mwandishi** wa Nipashe atunukiwa tuzo

UKURASA 7




**Klopp aelezea hali ya Van Dijk**

UKURASA 20

# Kina Mdee: Tuko tayari kwa lolote

• **Kukata** rufani kwa chama, mjadala mkali mitandaoni, Prof. Baregu afunguka... *Ukurasa 2*



Aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) Taifa, Halima Mdee (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kufutwa uanachama wa chama hicho na wenzake 18 na hatua wanazotarajia kuzichukua ikiwamo ya kukata rufani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wanafunzi 3,544 wapata mkopo bil.11/- awamu ya 3

UKURASA 7

## Majaliwa ataja sababu kushuka maambukizi VVU

UK. 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** **PLATEAU: TUTAPINDUA MEZA KIBABE** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Arusha, John Mwigura (katikati), akitoa ufafanuzi wa sakata la Shule ya St. Judy ya mkoani humo jana, ambayo wanafunzi wake wamelazimika kurudishwa nyumbani kwa madai ya kudaiwa kodi kubwa na mamlaka hiyo. Kulia ni Meneja Msaidizi makusanyo ya Kodi, Patrik Nyalobi na Meneja Msaidizi ukaguzi wa Kodi, Malaki Nyange. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# MDEE: Tuko tayari kwa lolote

**Na Elizabeth Zaya**

ALIYEKUWA Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), Halima Mdee na wenzake 18, wamesema wapo tayari kuachia ubunge, ikiwa mchakato wa rufani utafuata taratibu na kuwalazimu kufanya hivyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mdee aliyeambatana na wenzake 15 alisema watakata rufani kwa Baraza Kuu dhidi ya uamuzi wa Kamati Kuu ya CHADEMA iliyofikia uamuzi huo Jumamosi iliyopita.

"Whether yes or not (kama ndio au hapana) tutakuwa tayari ku-sacrifice (kujitoa) ubunge kutokana na vikao vyetu vya ndani na mchakato wa rufani ambayo tunafanya hivi sasa. Inawezekana chama kikabariki tukaenda ama tukatolewa wakaenda wengine, vyovyote itakavyokuwa," alisema.

"Katika chaguzi hizi zote tangu vyama vingi vimeanza, lakini zaidi kuanzia mwaka 2010, 2015 na 2020 hakuna uchaguzi ambao tuliukubali kwa sababu zote zilitawaliwa na taratibu ambazo ziko kinyume na sheria, lakini wabunge si walienda?" Alihoji Mdee.

"Sasa kama wabunge walienda 2010 na 2015 pamoja na kutokutambua, kwanini 2020 wasiende...kwa nini, kwa sababu tunavyozungumza sasa, madiwani wanaapa, mbunge mmoja aliyechaguliwa keshaapa, kwa hiyo mimi naamini kwamba suala siyo kwenda ama kutokwenda, kwa sababu siyo suala jipya, yalishafanyika huko nyuma."

"Kwa hiyo usishangae kama kesho na keshokutwa, iwe sisi ama wengine wakaenda kwa sababu ni kitu ambacho siyo kipya."

Kwa mujibu wa Mdee, CHADEMA hakikandamizi wanawake kwa kuwa walio kwenye nafasi hizo za uongozi na ubunge walijengwa na chama hicho mpaka kufika walipo.

"Siwezi kusema hapa kwamba chama changu kinakandamiza wanawake, wanawake mashoka unaowaona hapa ni kwa sababu walipewa nafasi na chama, wako hapa kwa sababu walijengwa na CHADEMA na siwezi kusema wanakandamizwa, hili limetokea kwa sababu."

Mdee alisema kuendelea kubaki wabunge au la kutakuja baada ya uamuzi wa rufani wanayotarajia kukata dhidi ya uamuzi ya Kamati Kuu.

Alisema yeye na wenzake wataendelea kuwa wanachama kwa sababu wanakithamini na kukipenda chama chao.

**TUHUMA KUNUNULIWA**

"Mimi ni mwana CHADEMA na nimekuwa mwanachama miaka 16 na katika muktadha huo pamoja na kwamba mimi na wenzangu tumechukuliwa hatua za kinidhamu, niwahakikishie tu kwamba mimi na timu yangu, tutabaki kuwa wanaCHADEMA kindakindaki."

"Sisi wote hapa tuna zaidi ya miaka mitano ya uanachama na kila mmoja ameshiriki kukijenga kwa jasho lake, niwahakikishie wanaCHADEMa nchi nzima, Halima mnayemfahamu miaka yote ni yuleyule na uaminifu wake na wenzake wote. Ninasema hivyo kwa sababu kumekuwa na maneno mengi kwamba nimenunuliwa kwa mpunga mrefu, mimi sijawahi kununuliwa na sitanunuliwa na sitarajii kununuliwa."

"Watu waliofanya kazi na mimi iwe kwenye chama, bungeni, wananjiua, ukiambiwa taja watu watatu ambao kwao rushwa ni mwiko, inawezekana nikawa namba moja na nikawa na wengine wanaonifanania hivyo, mimi sina thamani ya kipande cha fedha, kazi zangu zote nimekuwa nikifanya kwa uaminifu na kwa mapenzi toka moyoni, sina maigizo."

**KUITIKIA WITO**

Kuhusu kutokutii wito wa Kamati Kuu ya chama hicho, Mdee alisema walihofia usalama wao kutokana na ushawishi uliokuwa unafanywa kwenye mitandao ya kijamii iliyokuwa na mwelekeo wa kuwadhuru.

"Tulipata wito wa kutakiwa kuhudhuria kikao cha Kamati Kuu Novemba 27 saa mbili asubuhi, lakini kutokana na sintofahamu iliyojitokeza, Novemba 26, tulimwandikia barua Katibu Mkuu tukimuomba asogeze kikao mbele japo kwa wiki moja, na tulifanya hivyo kwa sababu utaratibu wetu wa kikatiba wa kawaida unaruhusu," alisema Mdee.

"Katiba inasema mtu anatakiwa kujulishwa makosa yake kwa maandishi na kutakiwa kutoa majibu katika muda usiopungua wiki mbili, apewe nafasi ya kujitetea mbele ya kikao kinachohusika na baada ya kujitetea, uamuzi utatoka ndani ya wiki mbili.

"Pia tarehe iliyopangwa kikao kulikuwa na uhamasishaji mkubwa sana kwenye mitandao ya kijamii, wengine ni viongozi wakiwaambia wanachama waje watushambulie na kutupiga mawe kwa sababu ni wasaliti, kwa hivyo sisi kama binadamu tusingeweza kuhudhuria katika kikao hicho, lakini siyo kwamba tulidharau chama."

Mdee alisema dhamira yake ni kutaka kila jambo limalizike na warudi katika hali ya kawaida.

Pia, alisema wataendelea kuwa wanachama wa hiyari kwa sababu wao na chama chao ni 'damudamu'

"Itoshe tu kusema kwamba tunakipenda CHADEMA tunakiheshimu, hatutaondoka, tutabaki wanachama wa hiyari mpaka pale tutakapokwenda kujadili mambo yetu ya ndani na kuyamaliza, kwa lugha nyingine sisi tutabaki wanachama 'ving`ang`anizi'."

"Kwa hiyo ninaamini kwamba Mungu atatuongoza na tutaenda kuyajenga ndani kwetu, siko hapa kwa ajili ya kuleta madhara yoyote kwa chama changu."

Katika mkutano huo, Mdee alikataa kujibu baadhi ya maswali aliyoulizwa hasa alipotakiwa kuweka wazi mchakato mzima uliotumika kupatikana wabunge hao 19 waliokwenda kuapa bungeni.

# Mjadala mzito hatima ya CHADEMA

**Na Elizabeth Zaya**

WACHAMBUZI wa siasa wamesema kwamba mvurugano unaoendelea ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), unahitaji maridhiano yanayozingatia misingi ya Katiba ya chama hicho.

Pia wamesema, siyo jambo geni na limewahi kutokea katika vyama vya siasa mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na Nipashe, wachambuzi hao wa siasa walisema bila kutulia na kufanya maridhiano hayo wanaweza kuwachanganya wanachama wao.

Selemani Bishangazi, mwanaharakati na mchambuzi wa masuala ya siasa, alisema chama chochote chenye wafuasi wengi hakiwezi kukosa migogoro isipokuwa ni kuwa makini kusimamia misingi na Katiba yake na kufanya hivyo kunaweza kukiimarisha zaidi.

"Masuala yanayotokea ndani ya CHADEMA siyo mageni, yanatokea hata nje ya Tanzania, yalishawahi kutokea ndani ya Chama cha Wananchi (CUF), Chama Cha Mapinduzi (CCM) na vyama vingine, kinachotakiwa ni kukaa na kufanya maridhiano na kuheshimu misingi ya Katiba za vyama vyao," alisema Bishangazi.

Prof. Abdallah Safari, alisema kinachotokea ndani ya CHADEMA ni uamuzi ambao unaweza kufanywa na chama kingine chochote, na kwamba kufanya hivyo kunaweza kuleta uimara zaidi katika chama.

"Unajua hili suala siyo geni, na ikumbukwe kwamba kila chama huwa kina misingi yake, tumeshuhudia pia CCM walikuja na utaratibu wake wa kuvua watu 'magamba' na pia wamewahi kuchukua hatua mbalimbali kwa wanachama wanaokwenda kinyume cha taratibu za chama chao, CUF, na vyama vingine nao waliwahi kufanya hivyo, hata huko duniani, kwa hiyo kilichofanyika CHADEMA, wameheshimu misingi na katiba yao," alisema.

"Na kawaida misingi ya vyama inapoheshimiwa ndiyo uimara wenyewe wa vyama."

Deusi Kibamba, alisema kinachotokea ndani ya chama hicho ni kukosekana kwa vikao vya kutatua matatizo yanayojitokeza ndani ya chama hicho na kinaweza kusababisha kuua chama kama ilivyowahi kutokea katika baadhi ya vyama vya upinzani.

**BAREGU ANENA**

Katika ukurasa wake wa Tweeter, Profesa Mwesiga Baregu, aliandika kuwa: "Maamuzi mazuri yanawezafanywa na Kamati Kuu kulingana na anayeongoza kamati husika."

"Mara ngapi Kamati Kuu zinatoa maamuzi yasiyo sahihi? Maamuzi mengi ya Kamati Kuu yanategemea maono ya kiongozi wake, naendelea kusema maamuzi ya Kamati Kuu chini ya Mbowe (Freeman) yalikuwa sahihi," alisema.

**MTANDAONI**

Kwenye mitandao ya kijamii, wananchi mbalimbali walikuwa wakichangia kwa mitazamo tofauti ya kuungano mkono uamuzi wa kuwawekea hao na wengine wakiwaita wasaliti wa demokrasia.

"BAVICHA Mkoa wa Mara tupo tayari kukilinda chama kwa gharama yoyote, Kamati Kuu imefanya maamuzi sahihi," ujumbe huo uliandikwa kwenye ukurasa wa Tweeter wa BAVICHA Taifa.

"Mdee anatakiwa kusema na kuweka wazi namna mchakato mzima ulivyokuwa mpaka wao wakapendekeza na chama kuwa wabunge na nani alipeleka majina yao Tume," aliandika anayejiita Myahudi.

"Kwa Press (mkutano na waandishi wa habari ), kweli nimeamini kuwa binadamu ni wadogo, tuliosimama kwenye mabega ya watu. Lakini kwa bahati mbaya tunajisahau na kuona tulipofika ni kwa uwezo wetu," aliandika David Mfungwa.

Naye, mwanahabari Privatus Karugendo, aliandika: "Hawa wanawake 19 wa CHADEMA, ninawafahamu vizuri, ninawaheshimu sana kwa msimamo wao na uaminifu mkubwa kwa chama chao na taifa lao. Ni kitu gani kimewapata? Fedha? Hapana! Ubunge? Hapana, hawa ni wapambanaji, watiifu na wazalendo! Wamejikwaa wapi? Halima! Niambie!

## HABARI KITAIFA




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiangalia mchoro unaoonyesha makisio ya watoto wanaoishi na VVU, kwenye banda la Kitengo cha Tiba na Mafunzo wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi (NACP), katika Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, yaliyofanyika kitaifa katika Uwanja wa Mandela, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, jana. **PICHA: OWM**

# PM ataja sababu kushuka maambukizi VVU

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amebainisha sababu za kupungua kwa vifo vitokanavyo na Ukimwi zikiwamo kuimarishwa kwa huduma za tiba hususan matumizi ya dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi (ARV).

Amesema vifo vitokanavyo na maradhi hayo vimepungua kutoka 85,000 mwaka 2001 hadi 21,529 mwaka jana.

Majaliwa aliyasema hayo leo katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kitaifa katika Uwanja wa Mandela Manispaa ya Moshi, kaulimbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ilikuwa 'Mshikamano wa Kimataifa, Tuwajibike Pamoja.'

Alisema mbali na kupungua kwa vifo hivyo, pia maambukizi mapya yamezidi kupungua kutoka watu 130,000 hadi 68,484 katika kipindi hicho, hivyo kutoa wito kwa wadau kuongeza jitihada zaidi.

"Mafanikio yote haya yametokana na kuendelea kuimarika kwa huduma za tiba ikiwamo matumizi ya ARV na afua za kinga zinazohusisha tohara ya kitabibu kwa wanaume na kuzuia maambukizo ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto," alisema.

Amesema Tanzania imefanikiwa kufikia malengo ya tisini tatu (90:90:90) hasa katika 90 ya pili na ya tatu.

"Kwa kujikumbusha tu ni kwamba tisini tatu zinalenga kuhakikisha kuwa asilimia 90 ya WAVIU wanajua hali zao; asilimia 90 ya wanaojua hali zao wanaanza kutumia dawa za kufubaza mapema na asilimia 90 ya walioanza dawa za kufubaza VVU kinga zao za mwili zinaimarika ifikapo mwaka 2023."

Kutokana na hali hiyo, alitoa wito kwa wadau wa mapambano dhidi ya VVU na Ukimwi, kuongeza jitihada hususani katika kuhamasisha upimaji wa VVU ili wafikie lengo la 90 ya kwanza.

**WITO KWA VIJANA**

Waziri Mkuu aliwataka vijana wajitambue na kuthamini maisha yao kwa kujikinga na maambukizi mapya ya VVU kwa kuwa wao ni nguvu kazi na taifa linawategemea.

"Vijana ni kundi linalokabiliwa sana na changamoto ya maambukizi mapya ya VVU nchini. Takwimu za maambukizi mapya ya VVU zinaonyesha kwamba asilimia 40 ya maambukizi hutokea kwa vijana na katika hao asilimia 80 ni vijana wa kike," alisema.

"Pia wale wanaoishi na VVU waendelee kutumia dawa za ARV kwa ufuasi sahihi bila kuacha ili waweze kufubaza VVU na kuimarisha afya zao," alisisitiza.

Kutokana na takwimu hizo, ni dhahiri alisema kundi la vijana, na hasa wa kike, liko kwenye hatari kubwa zaidi ya kupata maambukizi mapya kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kuanza ngono katika umri mdogo.

"Hali hii husababisha mhusika kuwa na uhusiano wa mapenzi na watu wengi hadi anapofikia utu uzima, hivyo, kujiweka katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU. Nawaasa vijana, msijihusishe na mapenzi katika umri mdogo. Ili vijana muweze kutimiza ndoto au malengo yenu katika maisha; ni lazima muwe na subira," alisema.

Waziri Mkuu amesema sababu nyingine ya vijana hao wadogo wa kike kuwa na uhusiano wa kingono na wanaume wenye umri mkubwa ni kuvutika na vishawishi kama vile pesa na zawadi ndogo ndogo.

**HALI KILIMANJARO**

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema kiwango cha maambukizi ya VVU mkoani hapa kimeendelea kupungua kutoka asilimia 7.3 mwaka 2004 hadi asilimia 2.6 mwaka 2017.

"Kiwango hiki kipo chini ya wastani wa maambukizi kitaifa ambacho ni asilimia 4.8. Hii haimaanishi kuwa tuko salama, hivyo sote tunapaswa kuongeza juhudi za pamoja ili tufikie lengo la maambukizi sifuri ifikapo 2030," alisema.

Balozi wa Marekani nchini, Dk. Donald Wright, aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa jitihada zake za kupambana na Ukimwi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa watu wote wanaoishi na virusi hivyo wanapata dawa, na kuahidi kuwa serikali yake itaendelea kushirikiana na Tanzania.

Awali, Mwenyekiti wa Baraza la Watu Wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (NACOPHA), Leticia Mourice, aliiomba serikali, asasi za kiraia, taasisi za dini na vyombo vya habari viendelee kutoa elimu ya makuzi, kubadili tabia na hofu ya Mwenyezi Mungu kwa vijana, wazazi na walezi ili kuwaepusha na matendo hatarishi.

• *Imeandikwa na Mary Mosha, MOSHI na Khadija Mussa (OWM).*

# Wanafunzi 22 wajeruhiwa na radi wakiwa darasani

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

WANAFUNZI 22 wa Shule ya Msingi De Paul Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, wamejeruhiwa vibaya baada ya kupigwa na radi wakiwa wanasoma darasani.

Habari zilizopatikana jana mchana mjini Songea ambazo zimethibitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, zimesema kuwa tukio hilo lilitokea saa 8.30 mchana kwenye eneo la shule hiyo, inayomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Songea.

Mkuu wa Wilaya Mgema alifafanua kuwa kati ya majeruhi 22, mmoja amelazwa katika chumba cha uangalizi maalum (ICU), huku wanafunzi 21 na mwalimu wao, Godfrey Kifaru, wakiwa wamelazwa kwenye wodi za kawaida wakiendelea kupatiwa matibabu katika hospitali ya serikali ya mkoa (HOMSO).

Alifafanua kuwa kati ya wanafunzi hao 22, wanafunzi 16 wa darasa la sita ambao walikuwa wanaendelea kusoma somo la Hisabati wakiwa wanafundishwa na mwalimu Kifaru huku wanafunzi wa 5 wa darasa la tano wakiwa kwenye darasa lao nao walipigwa radi na kujeruhiwa vibaya pamoja na mwanafunzi mmoja wa darasa la tatu.

Mgema amewatahadharisha wananchi katika msimu huu wa mvua kujihadhari na tabia ya watu kukimbilia kujificha chini ya miti kwani inaweza ikahatarisha uhai wao. Pia aliwataka wananchi wanapojenga nyumba zao kuweka waya wa kukinga radi ili kuepusha madhara.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Migwa, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo ambalo alisema ni la pili, na kwamba Novemba 25, mwaka huu majira ya mchana mvua ikiwa imeambatana na radi ambayo ilipiga kwenye ofisi ya mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wavulana Songea Boys na kuharibu thamani za ofisi ikiwamo meza ya ofisi ya mkuu wa shule, viti, makabati ya kuhifadhia kumbukumbu mbalimbali za shule na kusababisha kuvinjika kwa kuta na madirisha.

Mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Serikali ya Mkoa, Dk. Magafu Majira, alithibitisha kupokea majeruhi 23, ambao wanaendelea kupatiwa matibabu, na kwamba hali zao zinaendelea vizuri, isipokuwa majeruhi mmoja bado yupo chini ya uangalizi kwenye chumba cha wagonjwa mahututi.

**BAM INTERNATIONAL BV TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**MNADA WA HADHARA:**

UNIVERSAL AUCTION CENTRE Kwa idhini waliyopewa na BAM International Tanzania. watauza kwa mnada wa hadhara Makontena matupu, Mitambo ya ujenzi na vifaa vya ujenzi tarehe 5 December, 2020 siku za Jumamosi saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika BAM International eneo la mradi Batching Plant (Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere) Terminal 3 Dar es salaam.

**VIFAA VYA UJENZI NA FANICHA ZA OFISI ZITAKAZOUZWA:**
Mobile Fencing, Manhole covers, Aluminum Profile, Galvanized street light poles, Steel and aluminum Scaffoldings, Podium Ladder, Pipe hard insulations, Mesh, Electrical items, Welding rods, Knauf Insulation materials, Sandwich panels, Fire Fighting fittings, Hose & Valves, Ceiling Tiles, Floor Tiles, Canon Photo Copy m/c C5235, Plotter HP 520,File Cabinets, Office Table, Chairs, Construction Plastic Spacers, Armoured Cables, Vyuma Chakavu na vingine vingi.

**MAKONTENA NA MITAMBO YA UJENZI YATAKAYOUZWA KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI**

| Idadi | Aina | Model | Hali yake | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 47 | Empty Container 40FT. | High Cub, STD& Open Top | Nzuri | Umelipwa |
| 8 | Pipe welding/Threading m/c | 160mm | Nzuri | Umelipwa |
| 4 | Welding m/c 250/ Invater | 250 / 522 / 3- phase | Nzuri | Umelipwa |
| 2 | Table Saw machine | ZBV -450 | Nzuri | Umelipwa |
| 4 | Floor cutting machine | Honda | Nzuri | Umelipwa |
| 5 | Converter Poker Vibrator | LAIE 2 | Nzuri | Umelipwa |
| 3 | Multi stage pump | 11Kw / 15 - HP | Nzuri | Umelipwa |
| 4 | Terrazzo Grinding machine | 3 phase | Nzuri | Umelipwa |
| 12 | Assorted Terrazzo Machine | Vacuum cleaner/ Polish | Nzuri | Umelipwa |

Mali zote zitakaguliwa BAM International eneo la mradi Batching Plant JNIA T3 Dar es Salaam, Tarehe 3 mpaka 4 December, 2020 kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni

**MASHARTI YA MNADA:**
1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi kabla ya December 11,020 saa 10:00 jioni kwenye bank Akaunti ya BAM utakayoelekezwa, ukishindwa kulipa kwa muda huo mali itauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
3. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote.
4. Kila mtu atatakiwa kuwa na bid namba itakayo patikana getini,

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO. 5 "E" LION STREET SINZA DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926, E-mail: universalauction@hotmail.com**

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

KUMB: PPR/2020 - 12/1

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 2 DISEMBA 2020

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia Jumatano, **Tarehe 2 Desemba 2020.** Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Bei za rejareja na jumla za mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyopokelewa kupitia Bandari ya Dar es Salaam zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Novemba 2020. Kwa mwezi Desemba 2020, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 37/lita (sawa na asilimia 1.97) na Shilingi 47/lita (sawa na asilimia 2.71) na Shilingi 86/lita (sawa na asilimia 5.05). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli,Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa shilingi 37.36/lita (sawa na asilimia 2.11), shilingi 46.81/lita (sawa na asilimia 2.92) na shilingi 86.02/lita (sawa na asilimia 5.44),mtawalia.

(b) Kwa mwezi Desemba 2020, bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli kwa Mikoa ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimebadilika ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 4 Novemba 2020. Bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimepungua kwa shilingi 107/lita (sawa na asilimia 5.60) na shilingi 27/lita (sawa na asilimia 1.59). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei ya jumla ya Petroli na Dizeli imepungua kwa shilingi 106.40/lita (sawa na asilimia 5.99) na shilingi 27.28/lita (sawa na asilimia 1.71) mtawalia. Hata hivyo, bei za Mafuta ya Taa hazina mabadiliko na zitaendelea kuwa zile zilizotangazwa katika toleo la tarehe 4 Novemba 2020. Hii ni kwa sababu, kwa mwezi Novemba 2020 hakuna shehena ya Mafuta ya Taa iliyopokelewa kupitia bandari ya Tanga.

(c) Kwa mwezi Desemba 2020, bei za rejareja na jumla kwa bidhaa za mafuta ya Petroli na Dizeli kwa Mikoa ya Kusini (Mtwara, Lindi, and Ruvuma) zimebadilika ikilinganishwa na bei zilizotolewa tarehe 4 Novemba 2020. Bei za rejareja za Petroli na Dizeli zimepungua kwa shilingi 70/lita (sawa na asilimia 3.65) na Shilingi 4/lita (sawa na asilimia 0.25), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa shilingi 69.38/lita (sawa na asilimia 3.91) na Shilingi 4.32/lita (sawa na asilimia 0.27), mtawalia.

(d) Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (BPS Premium).

(e) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba *152*00# na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

(f) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

(g) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (price cap) kama ilivyokokotolewa na kanuni (formula) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 656 la tarehe 21 Agosti 2020.

(h) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.

(i) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (Electronic Fiscal Pump Printers) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

TANGAZO

# JEDWARI A: BEI ZA REJAREJA

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta Ya Taa (Shs/Lita) |
| **Dar es Salaam** | **1,865** | **1,687** | **1,621** |
| **Arusha** | **1,854** | **1,750** | **2,051** |
| Arumeru (Usa River) | 1,854 | 1,750 | 2,051 |
| Karatu | 1,872 | 1,768 | 2,069 |
| Longido | 1,865 | 1,761 | 2,062 |
| Monduli | 1,860 | 1,755 | 2,056 |
| Monduli-Makuyuni | 1,864 | 1,760 | 2,061 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 1,939 | 1,834 | 2,136 |
| **Pwani (Kibaha)** | **1,869** | **1,691** | **1,625** |
| Bagamoyo | 1,876 | 1,698 | 1,632 |
| Bagamoyo (Miono) | 1,907 | 1,728 | 1,663 |
| Chalinze Junction | 1,879 | 1,701 | 1,635 |
| Chalinze (Msata) | 1,883 | 1,705 | 1,639 |
| Kibiti | 1,885 | 1,707 | 1,641 |
| Kisarawe | 1,872 | 1,694 | 1,628 |
| Mkuranga | 1,875 | 1,696 | 1,631 |
| Rufiji | 1,892 | 1,714 | 1,648 |
| **Dodoma** | **1,924** | **1,745** | **1,680** |
| Bahi | 1,931 | 1,753 | 1,687 |
| Chamwino | 1,919 | 1,741 | 1,675 |
| Chemba | 1,950 | 1,772 | 1,706 |
| Kondoa | 1,956 | 1,778 | 1,712 |
| Kongwa | 1,921 | 1,743 | 1,677 |
| Mpwapwa | 1,925 | 1,747 | 1,681 |
| Mtera (Makatopora) | 1,942 | 1,764 | 1,699 |
| Mvumi | 1,930 | 1,752 | 1,686 |
| **Geita** | **2,030** | **1,852** | **1,786** |
| Bukombe | 2,019 | 1,841 | 1,775 |
| Chato | 2,051 | 1,873 | 1,807 |
| Mbogwe | 2,068 | 1,890 | 1,824 |
| Nyang'hwale | 2,045 | 1,867 | 1,801 |
| **Iringa** | **1,929** | **1,751** | **1,685** |
| Ismani | 1,934 | 1,756 | 1,690 |
| Kilolo | 1,933 | 1,755 | 1,689 |
| Mufindi (Mafinga) | 1,939 | 1,761 | 1,695 |
| Mufindi (Igowole) | 1,948 | 1,769 | 1,704 |
| **Kagera (Bukoba)** | **2,080** | **1,902** | **1,836** |
| Biharamulo | 2,055 | 1,876 | 1,811 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,097 | 1,919 | 1,853 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,102 | 1,924 | 1,859 |
| Muleba | 2,080 | 1,902 | 1,836 |
| Ngara | 2,068 | 1,890 | 1,824 |
| Misenyi | 2,089 | 1,911 | 1,845 |
| **Katavi (Mpanda)** | 2,073 | 1,895 | 1,829 |
| Mlele (Inyonga) | 2,092 | 1,914 | 1,848 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 2,066 | 1,888 | 1,822 |
| Tanganyika (Ikola) | 2,091 | 1,913 | 1,847 |
| **Kigoma** | **2,096** | **1,918** | **1,852** |
| Uvinza (Lugufu) | 2,109 | 1,930 | 1,865 |
| Buhigwe | 2,085 | 1,907 | 1,841 |
| Kakonko | 2,053 | 1,875 | 1,809 |
| Kasulu | 2,082 | 1,904 | 1,838 |
| Kibondo | 2,061 | 1,882 | 1,817 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **1,844** | **1,739** | **2,041** |
| Hai (Bomang'ombe) | 1,847 | 1,743 | 2,044 |
| Mwanga | 1,837 | 1,732 | 2,034 |
| Rombo (Mkuu) | 1,861 | 1,756 | 2,057 |
| Same | 1,830 | 1,726 | 2,027 |
| Siha (Sanya Juu) | 1,850 | 1,746 | 2,047 |
| **Lindi** | **1,848** | **1,746** | **1,680** |
| Lindi-Mtama | 1,853 | 1,751 | 1,698 |
| Kilwa Masoko | 1,872 | 1,770 | 1,655 |
| Liwale | 1,884 | 1,782 | 1,701 |
| Nachingwea | 1,868 | 1,766 | 1,709 |
| Ruangwa | 1,874 | 1,773 | 1,711 |
| **Manyara (Babati)** | **1,888** | **1,784** | **2,085** |
| Hanang (Katesh) | 1,899 | 1,794 | 2,095 |
| Kiteto (Kibaya) | 1,904 | 1,799 | 2,100 |
| Mbulu | 1,901 | 1,797 | 2,098 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 1,920 | 1,816 | 2,117 |
| **Mara (Musoma)** | **2,043** | **1,865** | **1,799** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 2,084 | 1,906 | 1,840 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,052 | 1,874 | 1,808 |
| Rorya (Shirati) | 2,087 | 1,909 | 1,843 |
| Bunda | 2,035 | 1,856 | 1,791 |
| Bunda (Kisorya) | 2,044 | 1,866 | 1,800 |
| Butiama | 2,040 | 1,862 | 1,796 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,089 | 1,911 | 1,845 |
| Tarime | 2,055 | 1,876 | 1,811 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 2,059 | 1,881 | 1,815 |
| **Mbeya** | **1,972** | **1,794** | **1,728** |
| Chunya | 1,981 | 1,803 | 1,738 |
| Chunya (Makongolosi) | 1,996 | 1,818 | 1,752 |
| Kyela | 1,988 | 1,810 | 1,744 |
| Mbarali (Rujewa) | 1,956 | 1,778 | 1,712 |
| Rungwe (Tukuyu) | 1,981 | 1,803 | 1,737 |
| **Morogoro** | **1,890** | **1,712** | **1,646** |
| Mikumi | 1,905 | 1,727 | 1,661 |
| Kilombero (Ifakara) | 1,928 | 1,749 | 1,684 |
| Kilombero (Mlimba) | 1,950 | 1,772 | 1,706 |
| Kilombero (Mngeta) | 1,939 | 1,761 | 1,695 |
| Ulanga (Mahenge) | 1,938 | 1,760 | 1,694 |
| Malinyi | 1,949 | 1,770 | 1,705 |
| Kilosa | 1,908 | 1,730 | 1,664 |
| Gairo | 1,908 | 1,730 | 1,664 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 1,900 | 1,722 | 1,656 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 1,890 | 1,712 | 1,646 |
| Turiani | 1,915 | 1,737 | 1,671 |
| **Mtwara** | **1,834** | **1,733** | **1,693** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 1,871 | 1,769 | 1,742 |
| Masasi | 1,851 | 1,749 | 1,719 |
| Newala | 1,855 | 1,754 | 1,725 |
| Tandahimba | 1,848 | 1,747 | 1,718 |
| Nanyamba | 1,848 | 1,747 | 1,718 |
| **Mwanza** | **2,015** | **1,837** | **1,771** |
| Kwimba | 2,033 | 1,855 | 1,789 |
| Magu | 2,023 | 1,845 | 1,779 |
| Misungwi | 2,009 | 1,831 | 1,765 |
| Sengerema | 2,047 | 1,869 | 1,803 |
| Ukerewe | 2,075 | 1,896 | 1,831 |
| **Njombe** | **1,957** | **1,779** | **1,713** |
| Njombe (Kidegembye) | 1,978 | 1,800 | 1,734 |
| Ludewa | 1,995 | 1,817 | 1,751 |
| Makambako | 1,950 | 1,771 | 1,706 |
| Makete | 1,988 | 1,810 | 1,744 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 1,955 | 1,777 | 1,711 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **2,038** | **1,860** | **1,794** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 2,038 | 1,860 | 1,794 |
| Kalambo (Matai) | 2,045 | 1,867 | 1,801 |
| Nkasi (Namanyele) | 2,051 | 1,873 | 1,807 |
| **Ruvuma (Songea)** | **1,920** | **1,818** | **1,744** |
| Mbinga | 1,933 | 1,831 | 1,778 |
| Namtumbo | 1,911 | 1,809 | 1,774 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 1,958 | 1,856 | 1,788 |
| Tunduru | 1,885 | 1,784 | 1,803 |
| **Shinyanga** | **1,994** | **1,816** | **1,750** |
| Kahama | 2,007 | 1,829 | 1,763 |
| Kishapu | 2,022 | 1,844 | 1,778 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 2,025 | 1,847 | 1,781 |
| Salawe | 2,008 | 1,830 | 1,764 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **2,035** | **1,857** | **1,791** |
| Busega (Nyashimo) | 2,028 | 1,850 | 1,784 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,038 | 1,860 | 1,794 |
| Maswa | 2,027 | 1,848 | 1,783 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 2,034 | 1,856 | 1,790 |
| **Singida** | **1,956** | **1,777** | **1,712** |
| Iramba | 1,968 | 1,789 | 1,724 |
| Manyoni | 1,940 | 1,762 | 1,696 |
| Itigi (Mitundu) | 1,956 | 1,777 | 1,712 |
| Ikungi | 1,951 | 1,773 | 1,707 |
| Mkalama (Nduguti) | 1,980 | 1,802 | 1,736 |
| **Songwe (Vwawa)** | **1,981** | **1,803** | **1,737** |
| Songwe (Mkwajuni) | 1,988 | 1,810 | 1,744 |
| Ileje | 1,985 | 1,807 | 1,741 |
| Momba (Chitete) | 1,990 | 1,812 | 1,746 |
| Tunduma | 1,985 | 1,807 | 1,741 |
| **Tabora** | **2,019** | **1,841** | **1,775** |
| Igunga | 1,973 | 1,795 | 1,729 |
| Kaliua | 2,038 | 1,860 | 1,794 |
| Ulyankulu | 2,032 | 1,854 | 1,788 |
| Nzega | 1,984 | 1,805 | 1,740 |
| Sikonge | 2,031 | 1,853 | 1,787 |
| Urambo | 2,032 | 1,854 | 1,788 |
| Uyui | 2,020 | 1,842 | 1,776 |
| **Tanga** | **1,798** | **1,693** | **1,994** |
| Handeni | 1,818 | 1,714 | 2,015 |
| Kilindi | 1,833 | 1,729 | 2,030 |
| Korogwe | 1,810 | 1,705 | 2,006 |
| Lushoto | 1,819 | 1,715 | 2,016 |
| Mkinga (Maramba) | 1,805 | 1,700 | 2,001 |
| Muheza | 1,802 | 1,698 | 1,999 |
| Pangani | 1,804 | 1,700 | 2,001 |

**JEDWALI B: BEI ZA JUMLA**

| | Petroli (Shs/Lita) | Dizeli (Shs/Lita) | Mafuta ya Taa (Shs/Lita) |
|---|---|---|---|
| DAR ES SALAAM | 1,736.90 | 1,558.88 | 1,493.91 |
| TANGA | 1,669.82 | 1,565.33 | 1,866.20 |
| MTWARA | 1,706.70 | 1,604.88 | - |

**Mha. Godfrey H. Chibulunje**
**KAIMU MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Tuwekeze zaidi kukabili virusi

WAKATI dunia ikiendelea kupambana na maradhi ya UKIMWI, Tanzania imetimiza miaka 37 ya jitihada za kukabiliana na ugonjwa huo. Hata hivyo hali bado si shwari kwa kuwa maambukizi mapya hayajadhibitiwa.

Mathalani, watu 72,000 wanaelezwa kuwa wanaambukizwa kila siku na hiyo ikimaanisha kuwa kuna kujamiiana kusikojali usalama na afya za wahusika ni taarifa ya serikali ya mwaka jana kwenye Siku ya UKIMWI Duniani.

Mambo yanakuwa mabaya zaidi kwa sababu wasichana na mabinti ni waathirika zaidi takwimu zikieleza kuwa vijana hao wenye umri kati ya miaka 14 hadi 35 ni wengi katika takwimu za maambukizi mapya.

Duniani nako hali si shwari , Jarida la Umoja wa Mataifa UN) la mwezi uliopita, linalinukuu Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto (UNICEF), kwamba hali ilikuwa mbaya kwa waatoto mwaka jana.

Kwa mujibu wa UNICEF, kila sekunde 100 (takribani dakika mbili) zinazopita kuna mtoto aliyeambukizwa Virusi vya UKIMWI (VVU) na kufanya idadi ya watoto wanaoishi navyo kufikia milioni 2.8.

Nasi tujiulize ni watoto wangapi hapa nchini wameambukizwa VVU? Wanaambukizwa kwa njia zipi? Na kuanzia hapo tuwe na mikakati.

Jan awakati wa maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani, Waziri Mkuu anasifu juhudi zilizofikiwa katika kukabiliana na janga hilo, akisema idadi ya vifo vya Wanaoishi na VVU (WAVIU) wamepungua kutoka 85,000 mwaka 2001 hadi 21,529 mwaka jana.

Aidha, anasema Tanzania imefanikiwa kufikia malengo ya tisini tatu (90:90:90) hasa katika 90 ya pili na ya tatu.

90.90.90 zinalenga kuhakikisha kuwa asilimia 90 ya WAVIU wanajua hali zao; asilimia 90 ya wanaojua hali zao wanaanza kutumia dawa za kudhibiti VVU mapema na asilimia 90 ya walioanza dawa VVU kinga zao za mwili zinaimarika ifikapo mwaka 2023, hayo aliyasema jana Kilimanjaro.

Mwaka jana kulikuwa na taarifa kuwa WAVIU walikuwa milioni.1.4 na kwamba waliokuwa wakihudumiwa kwenye mpango wa dawa za kudhibiti VVU za ARV, waliongezeka kutoka asilimia 22 za mwaka 2009 hadi asilimia 57 mwaka 2017.

Kwa upande wa Wizara yaAfya ilitoa taarifa ikieleza kuwa hadi kufikia Septemba mwaka jana, alikadiria kuwapo watu 1,252,205 kati ya wananchi 1,600,000 au sawa na asilimia 78.26, waliokwishapima na kufahamu hali zao za kuwa na VVU.

Kama taifa kuna jukumu kubwa la kulinda vijana na kuwapa elimu endelevu kuanzia shuleni na mitaani ili kuwaepusha na maradhi hayo.

Vijana wanachukulia poa na kuna madai kuwa wapo wanaosema kuwa kwa kutumia ARV mtu anaweza kuishi na maambukizi kwa miaka yote bila kuwa na changamoto yoyote.

Ikumbukwe kuwa matatizo ya magonjwa ya virusi si UKIMWI peke yake kuna COVID -19 pia.

Hivi karibuni Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia UKIMWI (UNAIDS), linatoa angalizo kwamba janga la COVID-19, linakwamisha harakati za kukabili UKIMWI na kwamba malengo yanaweza yasifikiwe.


Shirika la UNAIDS linaziasa nchi zijifunze kutokana na hasara ya kutowekeza vya kutosha katika mifumo ya afya na ziongeze hatua za kumaliza ugonjwa huo.

Kuna haja ya kupanua wigo wa huduma za VVU na afya ya uzazi pamoja na kuondoa sheria za kibaguzi, kunyanyapaa na kunazokandamiza wanawake ili kuwaepusha wasichana na mabinti na VVU.

Tunaona kuwa ni vyema kuwekeza kwenye afya na utafiti wa magonjwa ili kuwa na uwezo wa kupambana na maradhi ya milipuko kama UKIMWI na COVID-19.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Faustine Feliciane

# Ni zama za kutosikia tena mauaji ya wazee

MAUAJI ya binadamu kwa wazee, watoto wenye ulemavu au wafanyabiashara kwa namna yoyote ni ukatili uliozidi, unaostahili adhabu kisheria na kukomeshwa.

Karibuni kumekuwa na mauaji ya wazee yanayofanywa na baadhi ya watu huku kukiwa na sababu za 'kijinga' zinazowahusisha na ushirikina.

Pamoja na serikali na taasisi nyingine kukemea mauaji ya wazee katika maeneo mbalimbali hapa nchini hususani kwenye mikoa ya kanda ya ziwa kwa imani za uchawi, kusikia kuwa bado wanauliwa ni mambo yanayoongeza chumvi kwenye vidonda vya wazee.

Hivi karibuni kumeripotiwa taarifa za kuuawa wazee wilayani Igunga mkoani Tabora, ukiwa ni mwendelezo wa matukio kama hayo yanayotokea mara kwa mara ukanda wa ziwa na mikoa jirani.

Hili nalo ni la msingi kila binadamu ana haki ya kuishi, kulindwa, hivyo ni jinai kuukatisha uhai wa mtu kwa namna yoyote, labda kwa hukumu ya mahakama , hatua ambayo nayo inaendelea kuhojiwa na kupingwa popote dunia ikionekana kuwa kuua si adhabu stahiki.

Ndiyo maana kukomesha mauaji haya ni lazima sasa na mamlaka zinazohusika kufanya kazi kwa umakini na kuwakamata watuhumiwa wanaoendelea na mauaji ya wazee wasio na hatia. Miaka kadhaa iliyopita katika maeneo hayo na mikoa mingine jirani yalikithiri mauaji ya wenzetu wenye ualbino, serikali na wadau wa kitaifa na kimataifa ilipaza sauti na kuyakomesha.

Asasi zisizo za kiraia nazo zilipaza sauti na vyombo vya habari vilikemea vitendo hivyo vikapungua kutokana na watuhumiwa wanaopatikana na hatia kuadhibiwa.

Hivyo hakuna sababu ya kuwahurumia watu ambao wanawaua wengine kikatili hasa wazee hawa kwa sababu za kishirikina na nyinginezo, adhabu kali zitolewe kwao wanapopatikana na hatia bila kuangalia jina au nafasi zao kwenye jamii au familia.

Tanzania inasifika nje ya mipaka yake kuwa ni nchi ya amani na utulivu lakini inasikitisha pamoja na sifa inazozipata bado baadhi ya Watanzania wanauliwa wakati Mungu aliwapa baraka ya kuishi.

Ikumbukwe Watanzania hawa wanaouawa kikatili kila wakati hawana nchi nyingine ya kwenda zaidi ya hii ya Tanzania, wanayoishi na wanayofukuzwa, hivyo tuwaulize wauaji, mnataka wakaishi wapi?

Serikali isifumbie macho matukio kama haya. Nchi inaendeshwa kwa sheria, hivyo wale wote wanaopatikana na hatia ya mauaji kama haya wanapaswa kuchukuliwa hatua kali pindi wanapopatikana na hatia ya mauaji.

Adhabu kali inaweza ikawa fundisho kwa watu wengine kwenye jamii kuheshimu haki ya mtu kuishi, tena kuishi katika nchi yake.

Mamlaka mikoani Mwanza, Shinyanga, Geita, Simiyu na Tabora na maeneo jirani ziwajibike matukio haya yashughulikiwe na hatua zichukuliwe kwanza kukomesha na kuadhibu watuhumiwa.

Lakini, viongozi wa dini kwa nafasi zao wabadilishe fikra za watu wanapokuwa kwenye nyumba za ibada na kukemea ushirikina na imani za uchawi.

Wawakemee waumini wao kuendekeza tabia za ushirikina ambazo zinapelekea kufikia hatua ya kuuawa kwa wazee wasio na hatia.

Kama watu watafuatilia mafundisho ya dini zao kwenye ibada ni wazi watakuwa na hofu ya Mungu na kusaidia kukomesha mauaji kama haya ambayo hayakubaliki kamwe kwenye nchi hii ambayo msingi mkubwa ni kuheshimu haki za binadamu na utu wa mtu.

Watanzania wawe na hofu ya Mungu kwa kujiepusha na uovu kama kukata watu na mapanga na kuwaua, kukata viungo vya watu wenye ualbino, kuchukua sehemu za miili ya watoto au wenye ulemavu kwa madai yoyote yale kwani mafanikio ya maisha yanatokana na kazi si ushirikina.

## HABARI KITAIFA

# Wanafunzi wapya 3,544 kunufaika na mikopo ya bil.11/- elimu ya juu

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetangaza orodha ya awamu ya tatu yenye wanafunzi wapya 3,544 waliopangiwa mikopo wa Sh. bilioni 11.04 kwa mwaka wa masomo wa 2020/21.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, ilisema ili kupata taarifa za kina kuhusu mikopo waliyopangiwa, wanafunzi hao wanashauriwa kutembelea akaunti walizotumia kuomba mikopo kwa njia ya mtandao, maarufu kama Student's Individual Permanent Account (SIPA).

"Kufuatia (kutokana na) kutolewa kwa awamu hii ya tatu, hadi sasa wanafunzi wa mwaka wa kwanza 53,364 wamepangiwa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 173.29. Aidha, wanafunzi 69,625 wanaoendelea na masomo wamepangiwa Sh. bilioni 247.5 baada ya kufaulu mitihani yao ya mwaka 2019/20," alisema Badru.

Badru alisema baada ya kutangazwa kwa awamu ya tatu za upangaji mikopo, hatua inayofuata ni kufunguliwa kwa dirisha la rufani kwa siku saba kuanzia leo, ili kuwawezesha waombaji ambao hawajapangiwa mikopo au hawajaridhika na viwango walivyopangiwa, kuambatisha nyaraka za ziada kuthibitisha uhitaji wao.

Kwa mujibu wa Badru, katika kipindi cha rufani, wanafunzi watahitajika kutembelea mfumo wa olas.heslb.go.tz, kufuata maelekezo na kuwasilisha rufani zao kutoka popote walipo bila malipo yoyote kwa HESLB.

"HESLB inatoa wito kwa wanafunzi ambao bado hawajapangiwa mikopo na ni wahitaji, kutumia muda wa siku saba (07) za rufani kuwasilisha nyaraka sahihi ili hatimaye wapangiwe mikopo ya kuwawezesha kulipia gharama za masomo," alisema Badru.

HESLB ilianzishwa mwaka 2004 na kuanza kazi rasmi Julai, 2005 ili kuwawezesha Watanzania kupata elimu ya juu na kukusanya fedha za mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika.

# Mwandishi Nipashe atunukiwa tuzo

**Na Mwandishi Wetu**

MWANDISHI wa Habari Mwandamizi wa gazeti la Nipashe, Salome Kitomari, ametunukiwa tuzo ya mwandishi wa habari za haki binadamu kwa mwaka 2020.

Tuzo hiyo ilitolewa jana na umoja wa wanachama wa asasi zisizo za kiserikali zinazotetea haki za wanawake chini ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Tanzania (LHRC).

Kitomari alitambuliwa kutokana na kazi zake za uandishi wa habari zilizowezesha wanawake wengi kupata haki zao, huku wanawake wengine watano wakitambuliwa kwa kazi za kijamii ambazo zimesaidia wanawake wengi.

Wanawake hao ni Mhadhiri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Vicencia Shule, Pili Kuliwa wa Kilwa, Janeth Zakaria wa Biharamulo, Rose Njiro wa Arusha na Flora Massoi wa Morogoro.

Tuzo hizo zilifanyika katika maadhimisho ya kimataifa ya wanawake watetezi wa haki za binadamu Novemba 29, mwaka huu, na maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia zilizoanza Novemba 25 hadi Desemba 10.

Katika siku hiyo wanawake wa asasi hizo walikutana na kujadili wanawake hao watetezi wa haki za binadamu na mbinu za kuchukua kukabiliana na ukatili.

Pia, kuiamsha jamii kuwalinda wanawake dhidi ya ukatili, kuwawezesha wanawake watetezi kushiriki kikamilifu katika maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili na kutambua na kuwatia moyo wanawake vinara watetezi wa haki za binadamu kwa mwaka 2020.

Akizungumza wakati wa kukabidhi tuzo hizo, Ofisa Wanawake, Watoto na Watu Wenye Ulemavu, Getrude Dyabene, alisema wanawake hao wametambuliwa kwa kazi kubwa waliyoifanya kutetea wanawake na kupata haki zao.

"Katika kuadhimisha siku hii tulisema ni lazima tuwatambue wanawake wenzetu wanaofanya kazi nzuri, wamesaidia wengine bila kuchoka na kuvuta wengi, tunawatambua kwa mchango wao uliotukuka," alisema na kuongeza:

"Salome ni mwandishi wa habari ambaye ameandika habari nyingi za wanawake, amefuatilia kwa kina na ku-push (kusukuma) hatua zilichukuliwe na haki ipatikane kwa muhusika, na kupitia kazi zake wanawake wengi wamepata haki zao, ndiyo maana tumemtambua katika siku hii muhimu," alisema Dyabene.

"Lazima tuwasherehekee wenzetu, tuwape moyo kwa kitu kidogo, itawafanya wasonge mbele zaidi. Tuwekeze kwenye kueleza na kuweka kumbukumbu za mafanikio ya wanawake wenzetu, tusikubali tuongelewe tu nasi tuonyeshe tunaunga mkono," alisema.




Mwandishi Mwandamizi wa gazeti la Nipashe, Salome Kitomari, akifurahia tuzo aliyokabidhiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Tanzania (LHRC), Anna Henga (kulia), jijini Dar es Salaam juzi, iliyotolewa na umoja wa asasi zisizo za kiserikali zinazotetea wanawake katika maadhimisho ya siku ya kimataifa ya wanawake watetezi wa haki za binadamu na maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema bado kuna changamoto kubwa kwa watetezi wa haki za binadamu kutokana na fikra hasi dhidi yao.

Alisema bado jamii ina mtazamo hasi dhidi ya wanawake wanaotetea wengine kiasi cha kupewa majina mabaya na kunyooshewa vidole, huku wakionekana ni waliopotoka.

"Changamoto nyingine ni wale tunaowatetea wanabadili maamuzi na kumaliza kesi nyumbani, mtu alipigwa na kuumizwa, lakini anaamua kumaliza kesi nyumbani, na mtetezi anapofuatilia anaonekana amekosea, hii ni sababu ya unyanyasaji na matukio haya kuendelea," alisema.

Awali, vinara wa utetezi wa haki za binadamu wakitoa uzoefu wao, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Hellen Kijo Bisimba, Mkurugenzi Mtendaji wa Women Fund Trust, Mary Rusimbi na mmoja wa waanzilishi wa Mtandao wa TGNP, Asseny Muro, walisema watetezi wote bila kujali umri wanapaswa kushirikiana kutetea haki mbalimbali.

"Wakati wetu changamoto zilikuwa nyingi ila tulishikana kwa umoja wetu, tulijitoa na wengine waliacha kazi na kuwekeza kutetea haki za wengine," alisema Rusimbi.

"Mtazamo hasi bado upo kwenye jamii, wapo wanasidiwa mfano mwanamke alikatwa mkono na mume, mwingine alisukwa ghorofani akavunjika nyonga, watetezi tulifuatilia kwa karibu, lakini walivyoyamaliza hakuna aliyejua," alisema Bisimba.

Kwa mujibu wa Bisimba, watetezi wa haki za binadamu wanaume kwa sasa wana changamoto nyingi, ikiwamo kusingiziwa kuwa wana uhusiano wa kipenzi na wake zao.

Naye, Muro alisema rushwa ya ngono ilikuwa kubwa enzi zao, lakini walifanikiwa kuvuka kiunzi hicho kwa mbinu mbalimbali ikiwamo kushirikishana na kusimama pamoja.

# Watumishi wa hifadhi, mgambo jela kwa rushwa

**Na Joctan Ngelly, GEITA**

MAHAKAMA ya Wilaya Chato Mkoa wa Geita, imewahukumu wafanyakazi wawili wa hifadhi ya wanyamapori, wakala wa M-pesa na mgambo mmoja, kwa kosa la kuomba rushwa.

Washtakiwa wamehukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. 2,840,000 na kulipa fidia ya Sh. 9,500,000 kwa makosa manne ya kushawishi na kupokea hongo ya Sh. 9,500,000 kinyume na kifungu 15(1)(a) na (b) na kifungu kidogo cha pili cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Waliohukumiwa jana ni Omary Mazanza, Baraka Ukakale, ambao ni wote ni askari wa hifadhi ya wanyamapori pamoja na wakala wa M-Pesa Nicholaus Nyailala na mgambo, Alex Fransisco.

Washtakiwa kwa pamoja walishindwa kulipa faini hiyo na kupelekwa gerezani ili kuanza kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela.

Hukumu hiyo imetolewa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Erick Kagimbo, baada ya upande wa mshtaka kuthibitisha makosa yote manne pasipokuacha shaka yoyote.

Hakimu Kagimbo alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwao na kwa watu wengine wenye tabia kama yao.

Alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, ulipeleka mashahidi 11 na vielelezo tisa ambavyo vilithibitisha kuwa washtakiwa wote walitenda makosa hayo.

Alisema washtakiwa walikamata ng'ombe 22, mali ya Mutebuka Kanyamu katika eneo machungio na katika eneo la hifadhi ya akiba ya Chato, Burigi na Kimesi kisha kuzishikilia na kumshawishi mmiliki kutoa rushwa ya Sh. 9,500,000 ili kuziachia.

Hakimu huyo alisema washtakiwa wawili ambao ni askari wa hifadhi walimwelekeza mmiliki azitume fedha hizo kwa wakala wa M-pesa, anayeishi na kufanya biashara hiyo Ngara mkaoni Kagera.

Hakimu Kagimbo alisema: "Nimeangalia ushahidi wa pande zote na kugundua kuwa upande wa mashtaka umethibitisha makosa yote manne pasipokuacha shaka yoyote, hivyo basi washtakiwa wote mmetiwa hatiani kwa makosa yote mliyoshtakiwa."

Washtakiwa walijitetea kuwa wanaomba mahakama iwapunguzie adhabu kwa kuwa wana familia zinawategemea.

Baada ya washtakiwa hao kumaliza utetezi wao, upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa TAKUKURU, Murusuri alidai kuwa kwa vitendo vya rushwa vimekithiri katika maeneo ya hifadhi za wanyamapori na kurudisha nyuma juhudi za Rais Magufuli za mapambano dhidi ya rushwa, wanaiomba mahakama itoe adhabu kali dhidi ya washtakiwa hao ili iwe fundisho kwao na wafanyakazi wengine.

Hakimu Kagimbo alikubaliana na ombi hilo na kuwapa adhabu hiyo.

# Kortini madai ya kutoa taarifa za uongo Facebook

**Na Restuta Damia, BUKOBA**

TEOPHIST Mjuni mkazi wa Bukoba Mjini amefikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Bukoba Mjini mkoani Kagera, kwa madai ya kutoa taarifa za uongo kwenye mtandao wa kijamii wa Facebook kuwa meli ya MV Victoria ilizima ndani ya Ziwa Victoria mara tatu wakati ikitokea Bandari ya Mwanza kwenda mjini Bukoba

Wakili wa serikali, Emmanuel Kahigi, alisoma shtaka hilo Novemba 30, mwaka huu, mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, John Mpitanjia, na kudai kuwa Novemba 16 mwaka huu, mshtakiwa alichapisha taarifa za uongo ambazo zilileta taharuki kwa jamii.

Kahigi alidai kuwa taarifa hizo hazikuwa sahihi ambazo zilifanya jamii kupata mganganyiko.

Alidai kuwa meli ya MV Victoria Hapa Kazi tu ilizima mara tatu na meli ilizimika kwa nyakati tofauti ikitokea bandari ya Mwanza kwenda Bukoba na kwamba mtuhumiwa alishuka bandari ya Kemondo na kuchukua usafiri mwingine wa kumfikisha Bukoba.

Wakili wa serikali, Susan Maswea alidai kuwa, kesi hiyo imefika mahakamani kwa mara ya kwanza na kwamba upelelezi wake bado unaendelea.

Mshtakiwa huyo alikana mashitaka hayo na kuwa yuko nje kwa dhamana baada ya kukidhi masharti ya mahakama ambayo yalimtaka kuwa na wadhamini wawili ambao ni wakazi wa Bukoba na kila mmoja asaini bondi ya Sh. milioni tano na kesi hiyo itatajwa tena Desemba 14, mwaka huu.



Mwenyekiti wa Tume ya Madini nchini, Prof. Idris Kikula (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa mgodi wa dhahabu wa StamiGold, Mhandisi Gilay Shamika (kulia), alipotembelea maonyesho ya biashara na teknolojia ya madini, mjini Shinyanga, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**

# NBS yaokoa bil. 2/- sensa ya mifugo, uvuvi, kilimo

**Na Richard Makore, MWANZA**

SERIKALI kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), imeokoa Sh. bilioni tano ambazo zingetumika kufanya sensa katika sekta ya mifugo, uvuvi na kilimo iliyofanyika kati ya mwezi Agosti hadi Novemba, mwaka huu.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali kutoka Ofisi ya Takwimu ya Taifa, Dk. Albina Chuwa, alipozungumza na waandishi wa habari wakati akitoa matokeo ya sensa ya mwaka 2019/2020.

Dk. Chuwa alisema sensa katika sekta hizo mara ya mwisho iliyofanyika mwaka 2007/2008 na ilitumia Sh. bilioni 10, mwaka huu fedha hizo zimepungua kutokana na kuwapo teknolojia ya kisasa.

Alisema mwaka 2007/2008 kazi hiyo ilitumia muda wa miaka mitatu, ili kuikamilisha na kupata matokeo, mwaka huu wataalamu wametumia miezi miwili na nusu kukamilisha kazi yote.

Kwa mujibu wa Sheria ya Takwimu sura 351, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepewa mamlaka ya kuratibu na kusimamia takwimu zote rasmi za serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar.

Alisema sekta ya kilimo ina mchango mkubwa katika uchumi na maendeleo Barani Afrika na ni chanzo kikuu cha chakula kwa watu zaidi ya milioni 950 wanaoishi katika nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alisema kuwa takwimu za Benki ya Dunia (WB), mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa kwa nchi za Afrika ni asilimia 15.

Dk. Chuwa alisema nchi ya Afrika Kusini, ndiyo yenye mchango mkubwa zaidi wa sekta ya kilimo katika pato la taifa kwa asilimia 50.

Kwa upande wa Tanzania, Dk. Chuwa alisema, baadhi ya manufaa ya sekta ya kilimo ni pamoja na kutoa mchango kwa wastani wa asilimia 27.5, chanzo kikuu cha ajira kwa kuajiri zaidi ya asilimia 65 ya nguvukazi na chanzo kikuu cha fedha za kigeni kwa kuingiza wastani wa asilimia 24.7 ya fedha zitokanazo na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi.

Alifafanua kuwa sensa hii ni ya tano tangu Tanzania ipate uhuru na kwamba lengo ni kutoa takwimu sahihi na kwa wakati za kilimo, mifugo na ufugaji wa samaki, ambazo zitakuwa msingi wa kupanga, kufuatilia na kutathmini mipango ya kilimo pamoja na kutayarisha sera.

Matokeo ya sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi ya mwaka 2019/20 yanaonyesha kuwa, kaya milioni 7.8 sawa na asimilia 65.3 ya kaya zote nchini, zinajihusisha na shughuli za kilimo, kati ya hizo, milioni 7.7 kutoka Tanzania Bara na 180,219 ni kutoka Zanzibar.

Asilimia 65 ya kaya hizo, zinajihusisha na shughuli za kilimo cha mazao pekee, wakati asilimia 33 za kilimo na mifugo, na mbili ni ufugaji.

Matokeo ya sensa pia yanaonyesha kuwa, tani milioni 9.1 za mazao makuu ya chakula kwa upande wa nafaka zilizalishwa, mahindi yalikuwa tani milioni 5.7 sawa na asilimia 62.5 ya nafaka, ikifuatiwa na mpunga tani milioni 2.9 sawa na asilimia 32.1, mtama tani 488,724 sawa na asilimia 5.4.

Alisema sensa ya sekta hizo ya mwaka 2007/2008 ilionyesha kuwa uzalishaji wa mahindi ulikuwa tani milioni 5.4, mpunga 1.4 na mtama 552,354. Sawa na ongezeko la mahindi kwa asilimia 4.1, mpunga zaidi ya asilimia 100 na mtama umepungua kwa asilimia 11.5.

# Housigeli adaiwa kuua kwa kuambiwa ana roho mbaya kama sura yake

**Na Elizabeth Zaya**

MFANYAKAZI wa kazi za ndani Hapiness Sera (24) wa Kimara Korogwe Kinondoni jijini Dar es Salaam, anadaiwa kumuua Ezekiel Nyamko (24) kwa kumchoma kisu, baada ya kuambiwa kwamba ana roho kama sura yake.

Tukio hilo lilitokea Novemba 26, mwaka huu usiku katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kiipolisi wa Kinondoni, Ramadhani Kingai, mfanyakazi huyo wa ndani pamoja na aliyeuawa wote wanatoka Mkoa wa Mara.

"Ni kweli tukio limetokea Kimara Korogwe Novemba 26 saa tatu usiku, marehemu alikuwa ameenda kumtembelea rafiki yake anaitwa Kevin Tete ambao ni marafiki waliokuwa wamezoeana sana, lakini baada ya kufika nyumbani alikuta rafiki yake anaoga," alisema Kamanda Kingai.

"Akiwa amepumzika akaomba chakula kwa housigeli, ambaye alimkatalia kwamba hawezi kumpa kwa sababu wenyewe hawajala, labda asubiri baadae."

"Marehemu akamwambia hausigeli una roho mbaya kama sura yako ilivyo mbaya, ndiyo maana hata Kelvin hakuoi. Kwa hiyo akapata hasira na kumchoma kisu mara mbili upande wa kushoto, akadondoka akiwa anaomba msaada."

"Kelvin alivyotoka bafuni alikuta anagalagala chini, wakamchukua kumpeleka hospitalini, lakini kwa sababu alikuwa amemwagika damu nyingi alifia njiani."

Kamanda Kingai alisema baada ya Hapiness kufanya tukio hilo alikimbilia kwa majirani.

"Baada ya kuona amefanya tukio hilo alikimbilia kwa majirani, lakini tulimkamata na tunamshikilia," alisema Kingai.

"Na kwa sababu hii, tayari ni kesi, bado tunafanya uchunguzi kwa sababu ndio utaratibu wetu."

**"Akiwa amepumzika akaomba chakula kwa housigeli, ambaye alimkatalia kwamba hawezi kumpa kwa sababu wenyewe hawajala, labda asubiri baadae."**

# Kanisa laja na vitabu kuenzi kazi za JPM

**Na Edith Mruma**

KANISA Halisi la Mungu Baba, linatarajia kuzindua vitabu vitatu vya 'Ufahamu ulioanzia Tanzania kwenda mataifa yote' ukishirikisha viongozi wa serikali na taasisi mbalimbali za dini.

Akizungumza Dar es Salaam jana, kiongozi wa kanisa hilo, Baba wa Uzao, alisema washiriki kutoka nje na ndani ya nchi wameanza kuwasili kuhudhuria uzinduzi huo utakaofanyika Juamapili wiki hii Dar es Salaam.

"Kanisa Halisi la Mungu Baba tutakuwa na uzinduzi wa vitabu vitatu vinavyofahamika kama 'Ufahamu ulioanzia Tanzania kwenda mataifa yote' na tunatarajia viongozi mbalimbali wa serikali wakiwamo wabunge, taasisi za kidini na za kiraia kuhudhuria uzinduzi huo kwani hili ni suala la maendeleo ya kitaifa na kimataifa," alisema Baba wa Uzao.

**Kielelezo mojawapo cha kuonyesha kuwa nuru imeshukia Tanzania, ni kutokana na kuivusha kwenye mambo mbalimbali ikiwamo COVID-19.**

Alisema, lengo la vitabu hivyo ni kuelezea jitihada nzuri ambazo zimekuwa zikifanywa na Rais John Magufuli, hatua ambayo imeleta mabadiliko kwenye mfumo mzima wa maisha, lakini kuonyesha kwamba sasa nuru ipo Tanzania na ndiyo maana maajabu mengi yanazidi kutendeka.

"Kwa sasa ibada haiwezi kuwa ile tuliyozoea ya kwenda kuomba, bali ni kufanya kazi, ndiyo maana hata kaulimbiu ya serikali imebadilika na kuwa hapa kazi tu na hilo limekuwa likijidhihirisha kwa rais wetu, kwani tunamuona anafanya hayo kwa vitendo," alisema.

Alisema, kielelezo mojawapo cha kuonyesha kuwa nuru imeshukia Tanzania, ni kutokana na kuivusha kwenye mambo mbalimbali ikiwamo COVID-19.

"Mungu huyu aliyetushukia Tanzania hakuna vita tena kwenye nafsi zetu, imekuwa ni nchi ya nuru, kwani Tanzania leo imekuwa nuru kutokea nchini kwetu kwenda kwa mataifa mengine, kwa sababu sisi ni nchi pekee ambayo hatuna virusi vya corona duniani, jambo ambalo linafanya nchi nyingine kuja kujifunza kwetu na kutushangaa, haya ni maajabu ya Mungu," alisema.

Alisema hayo anayosema ni sauti ambayo imekuwa ikija mara kwa mara, hivyo vitabu vinavyokwenda kuzinduliwa vitaonyesha ni kwa namna gani nuru ipo Tanzania huku rais wetu akiwa ni kielelezo muhimu.

"Hata zamani kulikuwa na nyumba za ibada, lakini tafsiri yake ilikuwa ni kuwajibika kwa kutimiza majukumu yako vyema kama ni kulima basi lima, kama ni kufundisha basi timiza wajibu wako vizuri, hiyo ndiyo tafsiri ya ibada, ibada ni kufanya kazi kwa haki kwa ajili ya maendeleo ya watu na taifa kwa ujumla," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Masasi Mjini, Geofrey Mwambe, akizungumza na baadhi ya watumishi wa Shirika la Umeme (TANESCO), Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara jana, alipofanya ziara katika ofisi za shirika hilo, kwa lengo la kusikiliza changamoto zilizopo. **PICHA: HAMISI NASRI**

## GGM yajinadi mdau mkubwa ulipaji kodi

**Na Anthony Gervas,** GEITA

MGODI wa dhahabu wa Geita (GGM), umesema ni wadau wakubwa wa kulipa kodi za serikali kupitia sekta ya madini, hivyo kuchangia kiasi kikubwa katika uchumi wa taifa.

Akizungumza jana na Nipashe, mwakilishi wa mgodi huo, Erick Kalondwa, alisema kuwa mgodi huo unazalisha dhahabu kwa wingi pamoja na kusaidia sekta ya madini katika kuongeza utoaji wa ajira.

"GGM tunafanya kazi bega kwa bega na wanajiolojia na wataalamu wa sekta ya madini, ambao ndio wametusaidia kufikia hapa...sisi ni wadau wakubwa wa kuchangia kulipa kodi za serikali pamoja na kuongeza ajira kupitia sekta hiyo," alisema.

Kalondwa alisema kuwa mgodi huo umegundua migodi mingine mipya ya dhahabu katika mikoa ya Dodoma, Singinda na Shinyanga katika hatua za awali, baada ya kufanya utafiti wa madini. Alisema GGM itaendelea kufanya utafiti wa kugundua migodi mingine zaidi ya dhahabu ili kuongeza uzalishaji wake na ajira kwa Watanzania.

Alisema changamoto iliyopo hivi sasa katika mgodi huo ni biashara ya dunia ya dhahabu kuwa bei yake ikipanda na kushuka kila wakati, jambo ambalo limekuwa changamoto inayowakabili kiuzalishaji.

Alisema mikakati ya mgodi huo kwa sasa ni kuendelea kuleta matokeo chanya katika taifa, jamii, wabia, kuhakikisha unajiendesha, kuwapo usalama wa mazingira yanayowazunguka wananchi.

## Shinyanga watoa neno kupata mbolea

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

MBOLEA mpya aina ya MiCROP iliyozinduliwa mkoani Shinyanga imepokelewa kwa matumaini na wadau wa kilimo.

Mbolea hiyo imezinduliwa na kampuni ya YARA Tanzania, ambayo ni mzalishaji na muuzaji mkubwa wa mbolea nchini ili kusaidia wakulima wadogo wa mahindi na mpunga kupata mavuno mengi zaidi.

Akizindua bidhaa hiyo mpya mjini Kahama, mkoani Shinyanga mbele ya wanahabari, wakulima, maofisa wa serikali na wasambazaji, Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Kahama (KACU), Emmanuel Charahani, alipongeza ujio wa bidhaa hiyo mpya kwani itasaidia kuongeza uzalishaji miongoni mwa wakulima wadogo.

"Hii mbolea ni bora na pia iwasaidia sana wakulima wa mahindi na mpunga hapa nchini. Naomba nichukue nafasi hii kuwaomba YARA Tanzania kuja na bidhaa kama hii kwa ajili ya zao la pamba ili kuongeza uzalishaji," alisema Charahani.

Charahani ambaye ni Mwenyekiti wa Ushirika wa Vyama vya Tumbaku (TCJE), aliipongeza YARA Tanzania kwa ubunifu na dhamira yake ya kufanya kazi na wakulima sambamba na kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

"Mbolea hii mpya imekuja kipindi mwafaka, hivyo nawaomba wakulima wa mahindi na mpunga kuchangamkia fursa hii. Sisi Chama cha Ushirika Kahama tutaendelea kufanya kazi kwa karibu sana na YARA Tanzania kwa manufaa ya wanachama wetu na wakulima wote.

Kwa Meneja Biashara wa YARA Tanzania, Philipo Mwakipesile, alisema MiCROP ni mbolea ya kipekee kuzalishwa nchini pia fahari ya Tanzania kwa ukuaji wa sekta ya viwanda.

Mwakipesile alisema mbolea hiyo mpya ni ya kwanza kuchakatwa Tanazania na kampuni ya YARA ambayo itawasaidia wakulima wadogo kwani inavirutubisho vya Zinc na Sulphur Micronutrients zinahitajika kwa mazao yaweze kuwa na viwango bora.

"Tunajivunia kuzindua mbolea ya MiCROP hapa Kahama mkoani Shinyanga, ambapo wakulima wadogo wa mahindi na mpunga watapata fursa ya kuongeza mavuno sambamba na kuongeza mapato zaidi na chakula," alisema.

# Huawei yaigusa serikali juhudi kukuza TEHAMA

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Jim Yonazi, amepongeza juhudi za Huawei za kuboresha ubora wa elimu ya ICT ili kuongeza ujuzi wa kuajiriwa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Tanzania.

Dk. Yonazi alitoa pongezi hizo wakati wa ufunguzi wa msimu wa tano wa programu ya "Seeds for the Future" ambao ulifanyika mtandaoni mapema wiki hii. Kwa mara ya kwanza nchini, programu ya "Seeds for the Future" ilizinduliwa mwaka 2016 kwa msaada wa Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Programu hiyo ilihusisha vyuo vikuu 4 wakati ikizinduliwa na sasa inajumuisha vyuo vikuu 7 ambavyo ni Chuo Kikuu ya Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST), Chuo Kikuu cha Ruaha (RUCO), Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania (SAUT) na Chuo Kikuu cha Elimu cha Dar es Salaam (DUCE).

**Nimearifiwa kuwa katika kuchangia ukuzaji wa vipaji vya TEHAMA nchini na kuendana na mipango ya kimkakati ya nchi, Huawei imeongeza kwa kiasi kikubwa shughuli na ushirikiano na vyuo vikuu na vyuo vikuu hapa nchini.**

"Nimearifiwa kuwa katika kuchangia ukuzaji wa vipaji vya TEHAMA nchini na kuendana na mipango ya kimkakati ya nchi, Huawei imeongeza kwa kiasi kikubwa shughuli na ushirikiano na vyuo vikuu na vyuo vikuu hapa nchini. Hizi ni juhudi za kupongezwa kwa kuwawezesha vijana wa kitanzania," alisema Dk. Yonazi wakati akitoa hotuba yake kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Zainab Chaula.

Pia Dk. Yonazi aliwataka wanafunzi kutumia maarifa wanayopata kwenye programu hiyo kufundisha wengine ili kufaidisha idadi kubwa ya watu haswa wale ambao hawakuwa na bahati kama wao.

"Nawapongeza wanafunzi wote ambao wameshiriki katika programu ya Seeds for the Future mwaka huu. Nawashauri watumie fursa hii ipasavyo kukuza maarifa yao na kupata uzoefu wa vitendo katika TEHAMA. Ninawahimiza pia kushiriki uzoefu waliopata na wenzao ili kuendeleza na kunoa maarifa waliyoyapata," aliongeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Huawei Tanzania, Frank Zhou, aliangazia mipango ya Huawei ya kuiwezesha Tanzania kukabiliana na mahitaji ya teknolojia kidijiti ambayo yanabadilika mara kwa mara.

"Tunafahamu kuwa maendeleo ya dijiti yanahitaji mipango madhubuti ili kuiwezesha Tanzania kiuchumi kwa siku zijazo. Katika zama hii mpya, ujuzi wa TEHAMA utakuwa muhimu kwa jamii, kwa mashirika, na muhimu zaidi kwa vijana. Ndio maana tumewekeza kwa kina katika mipango kadhaa haswa ukuzaji wa vipaji na ujuzi," alisema.

Mwaka huu, ili kufikia vijana wengi zaidi Tanzania, Programu ya "Seeds for the Future" itafanyika mtandaoni ili iweze kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi kutoka mikoa tofauti na ili wanafunzi wenye mahitaji maalum pia washiriki. Ikilinganishwa na miaka ya nyuma, Huawei imeweza kuongeza idadi ya nafasi za mafunzo kutoka wanafunzi 10 hadi 47.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard aliisifia programu hiyo na nafasi yake katika kuwawezesha vijana na kukuza uwezo wa kuajiriwa.

"Programu hii ni mfano madhubuti wa ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Huawei Tanzania katika kujenga mazingira yenye afya na endelevu ya rasilimali watu katika TEHAMA. Inafanya kazi kama daraja ambalo linaunganisha pengo lililopo kati ya mafunzo ya kinadharia na mahitaji ya vitendo katika soko la ajira," alisema.



Naibu Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Mhandisi David Jere (kulia), akizungumza wakati wa mafunzo ya siku tatu kwa makandarasi wa Nyanda za Juu Kusini yaliyofanyika mkoani Njombe. Wa pili kulia ni Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Consolata Ngimbwa, Makamu Mwenyekiti wa Bodi, Joseph Tango na Meneja wa CRB Kanda ya Kusini, Ally Mwita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbunge akemea ufanyaji kazi kwa mazoea

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MBUNGE wa Masasi Mjini, Geofrey Mwambe, amezitaka sekta za elimu, afya, maji na nishati wilayani Masasi mkoani Mtwara kuacha kufanya kazi kwa mazoea badala yake wajikite katika kutimiza majukumu yao kwa uadilifu na kujituma zaidi, ili kuleta mabadiliko chanya.

Mwambe aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na watumishi wa sekta hizo kwa nyakati tofauti wakati wa ziara yake ya kikazi kwenye sekta ya afya, elimu na nishati, katika ziara ambayo alifuatana na wazee maarufu, madiwani wateule na viongozi mbalimbali wa serikali.

Awali akizungumza na watumishi wa Shirika la Umeme Tanznia (TANESCO) Wilaya ya Masasi, Mwambe alisema atahakikisha huduma ya umeme unaowafikia wananchi wengi zaidi katika vijiji vyao.

Alisema angependa kuona watumishi wa TANESCO wanafanya kazi kwa uweledi zaidi na kwa kujituma katika utoaji huduma ya nishati kwa jamii, na pale wanapokwama basi wawe wepesi kutoa taarifa ofisi ya mbunge ili kwa pamoja kutatua changamoto zinazojitokeza.

Mwambe alisema amesikitishwa kuona umeme wa REA kutofikia vijiji vingi katika Jimbo la Masasi, umeme hivyo wahusika waone umuhimu wa kulishugulikia jambo hilo na vijiji hivyo viweze kupata umeme.

**Nimesikitishwa kuona umeme wa REA kutofikia vijiji vingi katika Jimbo la Masasi, umeme hivyo wahusika waone umuhimu wa kulishugulikia jambo hilo na vijiji hivyo viweze kupata umeme.**

# Wiki mbili kwa manispaa kupeleka maji sokoni

**Na Vincent Tiganya,** TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, ametoa wiki mbili kwa uongozi wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kuhakikisha wamerudisha maji katika soko kuu.

Alitoa kauli hiyo jana wakati wa ziara yake ya kukagua masoko ya Tabora kwa ajili ya kujionea matatizo mbalimbali wanayokabiliana nayo wafanyabiashara.

Dk. Sengati alichukua hatua hiyo baada ya kutembelea soko kuu na kukuta maji yamekatwa na wafanyabiashara wa soko hilo wakiendesha shughuli zao bila ya kuwa na maji ya uhakika.

"Nataka hapa watu wapate maji ya uhakika ndani ya wiki mbili... angalieni katika 'strategic area' muweke maeneo ya watu kupata maji ambayo yatawasaidia kufanya biashara zao bila matatizo," alisema.

Dk. Sengati alisema utatuzi wa tatizo la maji katika soko hilo na mengine lazima ufanyike haraka ili kulinda afya za wafanyabiashara hao.


Aidha, aliuagiza uongozi wa Manispaa ya Tabora kukutana na viongozi wa masoko ili kuweka mpango endelevu wa kuhakikisha maji hayakatwi na mamlaka ya maji kwa sababu ya watumiaji kushindwa kulipia bili.

Katika hatua nyingine, Dk. Sengati ameuagiza uongozi wa Manispa ya Tabora kuhakikisha wanaweka umeme na kuziba nyufa paa katika soko kuu na Soko la Kachoma kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama wa bidhaa za wafanyabiashara hao katika masoko hayo.

Halima Mdee aking'ara mgongano wa chama, sheria, kanuni za bunge



Ukurasa 12



Ukurasa 14

DEBRETSION GEBREMICHAEL

siasa
JUMATANO DESEMBA 2, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# 'Sakata la wabunge 19 uje uchunguzi kuibua ukweli'

**Na Christina Mwakangale**

BAADA ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi mwaka huu CCM ilipata ushindi wa majimbo 258 kati ya 264 ambayo wabunge wake walipigiwa kura.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Dk Wilson Mahera, ananukuliwa akisema vyama vya upinzani vilipata viti nane kati ya 264, viwili Bara na sita Zanzibar.

CUF ilipata kiti kimoja, Mtwara Vijijini na Chadema kimoja Nkasi Kaskazini wakati Zanzibar ACT- Wazalendo ilipata viti vinne na CUF viwili, anaongeza.

Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi zinazotumia mfumo wa viti maalum vya wabunge wanawake, kwa mujibu wa sheria, hutenga viti maalumu kwa ajili ya wanawake ambao majina yao huwasilishwa EC na vyama vinavyofikia vigezo vya kisheria.

CHADEMA ilipata kura za urais wastani wa 1, 000,000 na kukifanya chama hicho kupewa nafasi ya kuwasilisha bungeni wabunge 19 wa viti maalum.

Lakini baada ya kuapishwa wabunge hao mjini Dodoma kumekuwa na mjadala kuhoji uhalali wa wabunge hao, huku chama kikizungumza na vyombo vya habari kuwa hakijafanya mchakato wa kuwapata wala hakihusiki.

Na ili kuthibitisha hilo kimewafutia uanachama wabunge wote 19 kuanzia wiki iliyopita.



Wabunge wa viti maalumu CHADEMA Easter Bulaya (kushoto) na Ester Matiko, wakila kiapo cha utii wiki iliyopita Dodoma.**PICHA: MTANDAO**

**TUTAJUAJE UKWELI?**

Kuna haja ya kufanya uchunguzi anasema mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Abbas Mwalimu, anapozungumza na Nipashe.

Mchambuzi huyu wa masuala ya kisiasa, anasema mivutano baina ya chama na wabunge hao, inaweza kuleta mpasuko katika chama.

Mwalimu anashauri kwamba kabla ya kuchukuliwa uamuzi na chama hicho, ipo haja ya kufanyika kwanza uchunguzi.

"Ili kujua tatizo limeanzia wapi wachunguze. Unaweza ukazima moto lakini chanzo cha moto bado kipo. Huenda yalifanyika mawasiliano ndani ya chama chenyewe," anashauri Mwalimu na kuongeza:

"Wajue changamoto zinatoka ndani au nje ya chama, vyama vyetu huwa vinafikiria kuwafuta uanachama.Unawezakuta Mdee anaondoka na kundi kubwa la watu, ukiangalia tena kuna wabunge wana ushawishi mkubwa."

Anafafanua kuwa suala lililopo ni mzozo wa kikatiba na kimamlaka na kwamba iwapo NEC inasema imepokea majina kutoka kwenye chama na bunge kutoka tume hiyo na kati ya walioteuliwa ni wabunge, ufanyike uchunguzi.

"Sidhani kama kuna athari za moja kwa moja kwa utendaji wa kibunge, ingawa kuwapo kwa wabunge wa upinzani kunaweza kuongeza vuguvugu bungeni.

CHADEMA ilipokutana na wanahabari ilisema Dar es Salaam, Katibu Mkuu John Mnyika, anasema kikao cha dharura cha Kamati Kuu, kikiongozwa na Mwenyekiti Freeman Mbowe, kilitoa uamuzi wa kuwafuta uanachama wabunge hao kwa kukiuka taratibu zake.

**ULINZI KISHERIA**

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Profesa Adelardus Kilangi, anawaonya CHADEMA kutowabugudhi wabunge hao wa viti maalum na kwamba mchakato wa kupata wawakilishi wa viti maalum kutoka CHADEMA umefuata sheria na katiba, hivyo hawapaswi kusumbuliwa.

Lakini Spika, Job Ndugai anasema, kanuni za bunge zinamtaka kuwalinda wabunge walio wachache na maslahi yao na kuahidi kufanya hivyo kwa nguvu zake zote.

Anasema kupatikana kwa wabunge hao kulifuata utaratibu kwa sababu alipokea majina ya wabunge wa viti maalum alipewa na na Tume ya Uchaguzi, na kazi yake ni kuwaapisha na kuwapa majukumu.

Anaeleza kuwa vyama viwili kati ya 20 vilivyoshiriki uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu ambavyo ni CCM na CHADEMA, ndivyo vyenye sifa ya kupata wabunge wa viti maalum kwenye bunge linaloanza kazi sasa hadi 2025.

Akizungumza jijini Dodoma, Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, anaeleza kuwa mkutano wa kwanza wa bunge idadi ya wabunge wa viti maalum hutokana na idadi ya kura za wabunge wote wa chama husika, ambapo chama kinatakiwa kupata asilimia tano ya kura zote halali za ubunge.

Aidha uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, CCM ilipata kura za ubunge milioni 8.3 wakati CHADEMA milioni 4.6 na CUF milioni 1.2. kutokana na kura hizo CCM ilipata viti 64, CHADEMA 36 na CUF 10.

Sakata hilo la viti maalumu linapokuwa na changamoto huleta fikra mbalimbali. Lakini cha msingi ni kufahamu kuwa nchi nyingi hutenga idadi ya viti vya wabunge kwa ajili ya kinamama wanaochaguliwa kwa namna tofauti.

Kuna mataifa ambayo wananchi hupiga kura mara mbili, kwanza kwa wawakilishi wao kwa jumla halafu kura ya pili kwa ajili ya wanawake peke yao.

Kuna pia mataifa ambayo yameanzisha majimbo ya uchaguzi kwa ajili ya wagombea wanawake pekee.

Viti maalum vya wanawake ni utaratibu unaopatikana katika nchi mbalimbali unaolenga kuongeza idadi ya wanawake katika bunge na mabaraza, hivyo ni jambo muhimu linaloongeza uwakilishi.

# Halima Mdee aking'ara mgongano wa chama, sheria, kanuni za bunge

Na Miki Taseni

MBUNGE wa zamani wa Kawe kwa vipindi viwili mfululizo, Halima Mdee, sasa anakuwa nyota wa aina yake katika uwanja wa siasa. Akiwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA) amejikuta katika mkondo wa kisiasa kugonganisha chama chake na uongozi wa bunge, ukiungwa mkono na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) pamoja na CCM.

Halima ni kama mwenyekiti wa kundi la wabunge 19 wanawake walioapishwa kwa nafasi za viti maalum upande wa CHADEMA, na ni wazi anayo nafasi maalum ya ushauri kwa wenzake kwenye timu hiyo.

Si rahisi kusema matokeo ya mvutano huo yatakuwa yapi, kwani inategemea wabunge hao walichoelewa wakati wanakula kiapo, aina ya ushauri walioupata, na mfumo wa kuungwa mkono au kuegemea wanakotegemea.

Kuna wasiwasi kama alichosema Mdee katika hafla ya kuapishwa kundi hilo (wabunge 19) kumpongeza Mwenyekiti wa chama Freeman Mbowe, ilikuwa ni taarifa sahihi ya kilichotokea, au 'alimbambikia' Mbowe.

Endapo kweli alipata baraka hizo, ina maana kwa njia moja au nyingine chama kitaendana na kilichotokea, halafu kauli ya kuwapa muda au kuwafukuzwa iote mbawa ni suala gumu.

Mpangilio ambao ungewafaa Mdee na wenzake ni mahali ambapo baada ya muda wa kuomba radhi kupita (kama upo) au kama kuna hatua ya kuwafukuza katika chama moja kwa moja, wafike mahakamani wapate zuio, halafu lidumu kwa muda wote uliobaki.

Kizuizi ni kama kuna ukomo wa zuio kama hilo kisheria na kama hata kesi ikianza kusikilizwa, inaweza kuzungushwa inavyotakiwa na huku wabunge hao wakiendelea siyo tu na kazi za ubunge, ila pia utambulisho wao CHADEMA.

Ila kuna kanuni ya kisiasa hapa nchini aliyoiweka Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, aliposema mwaka 1993 kuwa 'CCM siyo mama yangu,' kuwa endapo chama hicho kitavunja msimamo wa muungano wa serikali mbili, yeye atakuwa tayari kujitenga na chama hicho.

Kwa maana hiyo yako masuala muhimu katika maisha ya kisiasa yanayoweza kupunguza au hata kubatilisha utambulisho wa mtu kwa chama fulani, endapo 'nafsi yake itamsuta' kwa jambo hilo.

Kunukuu kauli ya Mwenyekiti wa CUF Profesa Ibrahim Lipumba, wakati 'akiachia ngazi' Julai 2015 baada ya ujio wa Edward Lowassa, akapewa bendera upinzani, alisema hakukubaliana na hatua hiyo, hivyo analazimika kuondoka.

Badala ya kuhangaika kungoja majibu katika mtiririko wa matukio, kuna haja ya kutumia 'kanuni ya kuisikiliza nafsi yako. Na kufanya yale unayoona inayakubali.

Ni hali halisi kwamba wabunge hao 19 wanawake wameapishwa na kwa maana hiyo hawatakuwa na dhamira ya jambo hilo kubadilika, libakie suala moja tu kuhusu uhusiano wao na chama cha awali, au utendaji wa chama kulingana na suala litakavyokwenda.



Halima Mdee, alipozungumza na wanahabari kuhusu kwenda mbele kukata rufani kupinga kufukuzwa CHADEMA. **PICHA: MTANDAO.**

> Kizuizi ni kama kuna ukomo wa zuio kama hilo kisheria na kama hata kesi ikianza kusikilizwa, inaweza kuzungushwa inavyotakiwa na huku wabunge hao wakiendelea siyo tu na kazi za ubunge, ila pia utambulisho wao CHADEMA.

Zuio la mahakama linaweza kuwa njia bora kwani baada ya hapo Spika atawalinda ibaki hivyo.

Jambo hilo hata hivyo halijasikika kwa nguvu kwani inategemea taratibu zinazofuatwa, kwa mfano kama nakala ya orodha ya wabunge wa viti maalum kulingana na kiwango cha kura alichopata mgombea urais wa chama hicho ilitoka CHADEMA au la. Endapo ilitoka CHADEMA haitakuwa rahisi kwa uongozi wa chama hicho kuithibitishia mahakama kuwa orodha iliyotolewa na Tume ya Uchaguzi haifahamiki kwao, ila tu hawataki kuwe na wabunge wa viti maalum kutoka chama hicho.

Viashiria vya hali kama hiyo vilishaanza kuonekana wakati mvutano ulipoanza kati ya CHADEMA na kundi la wabunge wa viti maalum, ikatoka habari inayopewa uzito wa kwanza na magazeti mbalimbali kuwa 'AG aionya CHADEMA.'

Ikisomeka kisheria, amri kuwa kusiwapo na wabunge wa CHADEMA katika Bunge la 12 ni uvunjifu wa sheria, hivyo inaweza kupuuzwa na mahakama, kuwa chama kinakuwa na uwezo wa kufukuza wabunge katika suala ambalo haligusi sheria ya uchaguzi.

> Viashiria vya hali kama hiyo vilishaanza kuonekana wakati mvutano ulipoanza kati ya CHADEMA na kundi la wabunge wa viti maalum, ikatoka habari inayopewa uzito wa kwanza na magazeti mbalimbali kuwa 'AG aionya CHADEMA.'

Na kwa maana hiyo kazi za uteuzi za tume na kanuni za bunge. Endapo upande wa Mwanasheria Mkuu utaihakikishia mahakama kuwa haki zote zinazotiririka kutokana na mahusiano hayo ya majukumu ndani ya sheria zilizingatiwa, kesi huenda ikaisha.

Kwa maana hiyo kuna mazingira ya kuwekwa 'precedent' uamuzi wa mahakama unaoweka kanuni mpya katika tafsiri ya sheria ambayo kwa maana hiyo itakuwa imefuta au imeongezea vipengele katika Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 na marekebisho yake.

Ni kuingiza kipengele cha tafsiri ya sheria kuwa chama kinaposhiriki uchaguzi kitakuwa kimetoa orodha ya umuhimu wa makada wake kwa uteuzi nafasi za viti maalum.

Na hivyo endapo chama kitakataa orodha hiyo kisipeleke majina Tume ya Uchaguzi, NEC itatumia nakala yake kufanya uteuzi. Halima Mdee naye pia ni mwanasheria, alisema nafasi hizo si zawadi ni stahiki kutokana na ushiriki wao na mapambano, halafu kijinsia ni kama uonevu, kuwa kwa vile wabunge wanaume ni kama hawapo, basi wakose wote.

SAKATA VITI MAALUM

# CHADEMA ni kama wanatwanga maji kwenye kinu - NGAWAIYA



Mwenyekiti wa CEGODETA, Thomas Ngawaiya (kulia) na Athuman Ali, alipoelezea mtazamo wa sakata la CHADEMA.
**PICHA: MPIGA PICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

KINACHOJIRI kwenye siasa za Tanzania kwa sasa, ni sakata la kufukuzwa uanachama, wabunge wa viti maalum wa CHADEMA, ambalo limekuwa gumzo kila kona.

Chama hicho kimewafuta uanachama kinamama wanachama wake 19 akiwamo Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake (BAWACHA) Halima Mdee, kutokana na kile kinachoelezwa ni utata wa upatikanaji wa majina ya wabunge hao waliokula kiapo wiki iliyopita bungeni Dodoma.

Yapo maoni mengi ambayo yametolewa na wadau mbalimbali kuhusu uhalali wa hatua hiyo, wakiwamo wanaosema kuapishwa kwao ni halali na wengine wakipinga.

Wakati sakata hilo likiendelea, Mwenyekiti wa Taasisi ya Maendeleo na Utawala Bora Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, anasema kufukuza watu uanachama si suluhu ya tatizo.

Ngawaiya mbunge wa zamani wa TLP Moshi Vijijini , aliyejiunga na chama hicho akitokea NCCR-Magezi, katika mazungumzo yake na gazeti hili jijini Dar es Salaam, anaeleza kuwa kuna mtego ambao CHADEMA hawana budi kunasa ili kufanikisha azma ya kutaka wabunge hao 19 waondoke bungeni.

"Kabla ya kuelezea hilo kwa kina, niseme kwamba, huu si wakati wa malumbano, ni wa maendeleo, hivyo CHADEMA waache wabunge wao walioapishwa wawatumikie wananchi kuliko hatua walizochukua za kuwafukuza," anawaonya.

Anafafanua kuwa wabunge wa Viti Maalum waliofukuzwa na chama hicho, bado ni wabunge halali hadi chama hicho kiandike barua kwa Spika ikiwa sababu zenye mashiko za kuwafukuza, kwa vile wana haki zao.

**CHADEMA MTEGONI**

Ngawaiya anasema, chama kipo mtegoni na kitanasa, hasa kwenye sakata la kutoutambua uchaguzi mkuu na kwamba kikiandika barua kwa Spika kuelezea hatua za kuwafukuza wanachama wake 19, kitakuwa kimemtambua na kukubali matokeo ya uchaguzi mkuu.

"Kwa maana hiyo, wabunge hao wataendelea kushiriki vikao vya bunge kama kawaida hadi hapo Spika atakapopata barua ya chama hicho ya kuwavua uanachama, lakini wakifanya hivyo maana yake wanautambua uchaguzi mkuu na ushindi wa CCM ambao wanaupinga," anasema.

"Ndiyo mtego ambao unasubiri kuwanasa CHADEMA kwa ajili ya kufanikiwa katika lengo lao la kuwatoa bungeni wabunge 19 wa viti maalum.

Suluhisho si kususa ama kufukuza wanachama au kutoingia bungeni, bali ni kushirikiana na serikali kwa vile uchaguzi umekwisha na sasa yaanze maisha baada ya uchaguzi," anasema Ngawaiya.

Anasema, CEGODETA inaamini kuwa, wabunge wa upinzani wanapoingia bungeni ama katika mabaraza ya uwakilishi, watapata nafasi ya kueneza sera zao na kutoa msimamo wa masuala mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

"Sisi tunaojihusisha na utawala bora, tumeona ni vyema tuwashauri viongozi wa upinzani wasiendelee kugoma na ikumbukwe wote nia yetu ni kujenga Tanzania, hivyo tushirikiane badala ya kugawanyika kwa sababu ya itikadi za kisiasa," anasema Ngawaiya.

Ngawaiya anasema, ili CHADEMA kujinasua katika mtego huo, ni kutambua matokeo ya uchaguzi mkuu kuliko kulalamikia kwenye vyombo vya habari kuhusu uapishwaji wa wabunge 19.

> "Sisi tunaojihusisha na utawala bora, tumeona ni vyema tuwashauri viongozi wa upinzani wasiendelee kugoma na ikumbukwe wote nia yetu ni kujenga Tanzania, hivyo tushirikiane badala ya kugawanyika kwa sababu ya itikadi za kisiasa," anasema Ngawaiya.

**WANAZUNGUKANA**

Baraza la Wazee la CHADEMA (BAZECHA), Mkoa wa Dar es Salaam, linaishauri Kamati Kuu kufanya uchunguzi wa kina kubaini waliohusika katika mchakato wa kuwapata wabunge hao 19.

Kwanza, wanaunga mkono hatua iliyochukuliwa na kuwavua uanachama wabunge hao, kwa madai ya usaliti, lakini pia ufanyike uchunguzi wa kina zaidi kubaini 'virusi' vyote vilivyoshiriki mchakato huo.

Hiyo ni kauli ya mwenyekiti wa baraza hilo Uhuru Kitima, wakati akizungumza na wanahabari, kwamba hawataki kuona wanaendelea kuwa na wasaliti ambao ni virusi ndani ya chama chao, hivyo ni bora wachunguzwe na wachukuliwe hatua kali, hata kama ni vigogo kwa kuwa nao ni sehemu ya wasaliti.

"Si vema kuacha watu wa namna hiyo ndani ya chama kwa sababu tayari wamekinajisi na baraza limesikitishwa na kulaani vikali kauli iliyotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya wabunge hao 19 na tunashangaa kuingilia kazi ya vyama vya siasa wakati yeye siyo mwanasiasa wala kiongozi wa chama chochote cha siasa," anasema Kitima.

Anaeleza kumshangaa kutoa tamko la kuzungumzia suala la viti maalum vya wanachama wake 19 na kwamba hatua kuingilia uamuzi wa chama si sahihi wakati yeye si kiongozi wa chama.

**NI WABUNGE HALALI**

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Job Ndugai anasema, wabunge wote wa bunge la 12 walioapishwa wanaendelea kutambuliwa kuwa ni wabunge kamili wakiwmo 20 wa CHADEMA, mmoja akiwa wa jimbo.

''Nashangaa wanawasonga tu hawa 19 yule mmoja wamemgwaya? Wakiweza wamfukuze basi, lakini sisi tumeshamwapisha na tunamtambua kwamba ni mbunge, hayo yanayoendelea huko ni ya kwao", anasema Spika Ndugai.

Akizungumza mara baada ya kuwaapisha wabunge wateule Humphrey Polepole na Riziki Lulida, anawatoa wasiwasi wale waliokuwa wakifikiri kuwa wabunge 19 wateule si halali, na kufafanua kuwa ni wabunge kamili.

Spika Ndugai anafafanua zaidi kuhusu sakata hilo kwa kusema; "Wabunge 19 ni kamili labda wao wenyewe waamue kwa kutumia utaratibu wa kikatiba kujiuzulu."

**MTAZAMO WA MSEKWA**

Spika mstaafu Pius Msekwa anasema, uamuzi wa chama hicho kuwavua uanachama wabunge 19 hauwezi kumpa ugumu Spika Ndugai kwa kuwa ni kama daktari anayepokea wagonjwa kuwatibu kisha wanaondoka.

Anasema hayo akizungumza na EATV&EA Radio Digital, kufuatia sakata la wabunge hao la kula kiapo cha ubunge bila ridhaa ya chama, kwamba, kama hawana chama kilichowapeleka bungeni, hata ubunge wao unakoma.

"Spika Ndugai hapati ugumu wowote, wanapoondolewa, yeye ni mpokeaji tu, hana ugumu na wala hafaidiki na lolote, ni kama mganga wa hospitali, anapokea wagonjwa akiwatibu wanaondoka, wakifa wanaondoka, hana jukumu zaidi ya hilo," anasema Msekwa.

# DEBRETSION GEBREMICHAEL

- Fundi mitambo anayelitesa jeshi na serikali ya Ethiopia
- Ana ‘jambo lake’ na serikali ya Abiy, aliutaka uwaziri mkuu



**Na Gaudensia Mngumi**

MPIGANAJI wa msituni au ‘gerila’ aliyekuwa kitisho kwa serikali ya Ethiopia, wakati huo akiwa kinara wa kuingilia na kukata mawasiliano ya Jeshi la Ethiopian, Debretsion Gebremichael, safari hii inaibuka tena kuwa mwiba kwa jeshi hilo na serikali yake.

.Mpiganaji huyo wa msituni ndiye kinara wa mtafaruku unaoendelea baina ya Jeshi la Ethiopia linaloongozwa na Serikali ya Waziri Mkuu Abiy Ahmed.

Debretsion anang’ang’ania na kulazimisha uhuru na kujitawala wa jimbo la kaskazini la Tigray, jambo linalopingwa mchana na usiku na Abiy.

Ukanda huo wa Tigray unaochukuliwa kama roho au mtima wa Ethiopia unataka kujitenga ili kula na kunufaika na rasilimali zake nyingi, japo ni maskini kupindukia.

Gebremichael anaongoza jeshi la ‘Watgiri’ la Tigray People’s Liberation Front (TPLF), chama kinachoongoza jimbo hilo.

Historia inaeleza kuwa kiongozi huyo ana damu ya uanamapinduzi tangu akiwa mtoto na inaeleza kuwa aliacha masomo katika Chuo Kikuu cha Addis Ababa miaka ya 1970 na kujiunga na TPLF akiwa na miaka 17.

Mpigajani huyo wa msituni wakati huo aliingia mitini kukabiliana na Waziri Mkuu wa Ethiopia aliyekuwa akiunga mkono sera za kikomunisti za Marx, Mengistu Haile Mariam.

Alikuwa miongoni mwa mawaziri wa nchi hiyo baada ya kuangushwa kwa Haile Mariam, lakini alishindwa na kuangushwa na muungano wa vyama vilivyoongozwa na chama cha TPLF, hadi Waziri Mkuu wa sasa Abiy Ahmed aliyeingia madarakani mwaka 2018.

**NI FUNDI MITAMBO**

Akitokea kwenye familia ya waamini wa madhehebu ya ki-Orthodox, kiongozi huyo wa Watigrei, anafahamika kama Debretsion, jina linalomaanisha Mlima wa Sayuni (Zion) na jina la baba yake Gebremichael, likimaanisha mtumishi wa Mtakatifu Michael.

“Akiwa shule ya msingi alikuwa akikusanya betri za redio, redio mbovu, vifaa vya umeme na kuvitengeneza na cha kushangaza wakati tulikuwa tukiishi gizani mtaani kwetu alitengeneza balbu kutokana na vitu hivyo alivyokusanya” anasema rafiki yake wa karibu Alemayehu Gezahegn.

> “Tigray ni hazina, ni sehemu ya historia ya taifa letu ilipoandaliwa na ni eneo ambalo wavamizi wa kegeni wakiwamo Waitalia na Wamisiri walishindwa katika mapigano na kuaibishwa na majeshi yetu. Kwa taifa letu tunapaheshimu na kupachukulia kama mtima wa nchi yetu” anasema Waziri Mkuu Abiy mwaka 2018.

Anaongeza kuwa baada ya kuhitimu shule ya mafunzo yao ya kijeshi walikubaliana kuwa kutokana na uwezo wake mkubwa kwenye ufundi apelekwe kwenye idara ya ufundi ya chama cha TPLF.

Gebremichael, ilikuwa kinara kwenye ufundi akitekeleza jukumu kubwa la kuweka mfumo wa taarifa za kiintelijensia na utaratibu uliowezesha jeshi la chama cha TPLF kudukua na kusikiliza mawasiliano na taarifa za wajeshi wa Ethiopia wakati wa mapigano.

Kuingilia pamoja na kukata mawasiliano yao ya redio kulililimaliza jeshi la serikali.

“Hii ilisaidia ushindi kwa upande wetu maana wapiganaji wa TPLF walifahamu kuhusu maadui zetu na nyendo zao kabla hawajafanya shambulio kwani tulikata mawasiliano yao, hatua iliyowasababishia kushindwa kuwasiliana kila waliposhambuliwa na ukawa mwanzo wa kushindwa” anasema Alemayehu.

Ili kutimiza azma ya kuwa mkuu wa mawasiliano kwenye vikosi vya chama na kuongeza ujuzi Debretsion, alitumia pasi bandia ya kusafiria na kuingia Italia na kujipatia mafunzo aliporejea alianzisha kituo cha matangazo cha redio cha TPLF’ kilichopewa jina la Dimtsi Weyane, ikimaanisha sauti ya mapinduzi.

Mpiganaji huyo wa msituni wa TPLF pamoja na wenzake kutoka timu ya mawasiliano walikuwa wanapandisha milimani usiku wa manane wakijua kuwa si rahisi kuonekana na majasusi wa jeshi la Ethiopia kufunga antena na minara za redio yao.

**MALUMBANO NA ABIY**

Debretsion na Waziri Mkuu Abiy walionekana kuwa marafiki na watu wanaoelewana wakati alipoanza kazi ya uwazi mkuu mwaka 2018. Kiongozi huyo wa Tigray, aliandaa mkutano wa makaribisho kwa Waziri Mkuu kutembelea makao makuu ya jimbo hilo huko Mekelle.

“Tigray ni hazina, ni sehemu ya historia ya taifa letu ilipoandaliwa na ni eneo ambalo wavamizi wa kegeni wakiwamo Waitalia na Wamisiri walishindwa katika mapigano na kuaibishwa na majeshi yetu. Kwa taifa letu tunapaheshimu na kupachukulia kama mtima wa nchi yetu” anasema Waziri Mkuu Abiy mwaka 2018.

**ANATAKA UWAZIRI MKUU**

Debretsion ni mpinzani wa Abiy na kuna wakati alinukuliwa na vyombo vya habari akisema “nilimwambia Abiy wewe ni mchanga. Hujakomaa kisiasa si mgombea unayefaa’”

Japo alisifia juhudi za Waziri Mkuu kutafuta amani na Eritrea na kupatana na Rais Isaias Afwerki, kumaliza vita ya maneno vilivyoanza tangu mwaka 1998-2000.

“Abiy alisafiri kutoka Eritrea na kukutana na Isaias. Hili lilishindikana kwa miaka mingi na ikawa ni fursa kwa taifa na kwa watu wake” alisema Debretsion.

Pamoja na kumsifia na kumfagilia, ukweli unabaki kuwa kiongozi wa Watigrei Debretsion alikuwa na nia ya kugombea uwaziri mkuu lakini akashindwa na Abiy mwaka 2018 akigombea kupitia muungano wa vyama.

Kushindwa kwake halikuwa jambo la kushangaza kwa vile TPLF ilikuwa ni sehemu ya ukandamizaji , ulaji rushwa na katika miaka 27 ya uongozi.

Tigray ina utajiri wa vitu vingi vikiwamo vya kihistoria kama makao makuu wa Ufalme wa Aksum , unaoelezwa katika historia ya Afrika kuwa ilikuwa ni eneo kubwa la ustaarabu duniani ikiwa ni miongoni mwa madola makuu ya wakati huo pamoja na Roma na Uajemi.

Magofu ya jiji la Aksum ni moja ya sehemu za urithi wa dunia yaliyotangazwa na Umoja wa Mataifa

.Baadhi ya vitu vya kihistoria ni pamoja na umri ikikadiriwa kuwapo kuanza karne ya kwanza hadi ya 13 baada ya Masiha Yesu Kristo.

Vilivyosheheni ni pamoja na ngome, makaburi, makanisa ikiwamo nyumba za ibada.



## Shirika lashauri walimu Chamwino

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI wa Shirika la Uwezo Tanzania, Zaida Mgalla, amewashauri walimu wakuu wa shule za msingi wilayani Chamwino zilizonufaika na mradi wa Jifunze, kuongeza siku 30 ili kumaliza idadi ndogo ya watoto waliobaki katika shule hizo ambao hawajui kusoma na kuhesabu.

Shule za majaribio zilizonufaika na mradi huo unaotekelezwa na Shirika la Uwezo Tanzania kwa kushirikiana na Women Wakeup ni Mwiyendaje, Chilonwa, Mkongonela, Chiboli na Amani.

Akizungumza na Nipashe jana, Mgalla alisema shule hizo zinapaswa kuendelea na utaratibu wa utekelezaji wa mradi huo kwa sababu vifaa ambavyo vinatumika kuwafundisha wanafunzi wa aina hiyo bado wanavyo hivyo hakuna sababu ya kusubiri msaada wa shirika ilhali wameshapewa mbinu za kufundisha.

Alisema kinachotakiwa ni kuangalia namna ya sera ya ufundishaji katika shule zao inasemaje na wao kutenga muda walau wa saa mbili kuhakikisha katika kila darasa wanafuta kabisa watoto wasiojua kusoma wala kuandika.

"Naomba endeleeni kuwafundisha wanafunzi waliobaki, kwa sababu dhana za ufundishaji mnazo, elimu pia mnayo fanyeni hivyo, ili mwakani shule zisiwe na watoto wasiojua kusoma isipokuwa darasa la kwanza wanaoandikishwa," alisema Mgalla.

Alisema walimu wanapaswa kukubaliana kwa pamoja namna ya kufanya kazi hiyo, ndani ya saa mbili au tatu ili jitihada ya kufuta ujinga katika shule hizo na nyingine zisififie.

Alisema kutokana na mradi huo kutekelezwa katika wilaya hiyo na umeleta matokeo chanya, mwakani anahitaji kusikia shule za msingi za Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino hazina wanafunzi wasiojua kusoma wala kuhesabu.

"Nawaomba mjitahidi mpango wa Jifunze usife kwa sababu kila kitu mnacho, mnapaswa kuendeleza ili Chamwino iwe mfano wa kuigwa na shule nyingine," alisema Mgalla.

Naye Mwalimu John Mrina, mmoja wa walimu wa wanufaika na mradi wa Jifunze, alisema, mafunzo hayo yamewasaidia kwa kiasi kikubwa kupata mbinu rahisi za kufundisha wanafunzi wasiojua kusoma na kuhesabu.

Alisema kabla ya kupata mbinu za kufundisha kutoka kwa watekelezaji wa mradi huo, ilikuwa tatizo kumtoa mwanafunzi katika hatua ya kutokujua kusoma na kuhesabu ili afanane na wanafunzi wengine, lakini sasa uwezekano huo upo.

"Tunashukuru sana Uwezo Tanzania na WOWAP wametusaidia kutupa mbinu za kufundishia wanafunzi waliokata tamaa kutokana na kutokujua kusoma, mbinu tunazotumia na vifaa vya kufundishia vinawafanya wanafunzi kuelewa haraka," alisema Mwalimu Mrina.

# Waliohujumu ushirika watakiwa kujisalimisha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewataka watu waliohujumu mali za vyama vya ushirika kujisalimisha na kuzirudisha kwa hiari kabla ya kuchukuliwa hatua na mali zote kurudi kwenye mikono ya serikali.

Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema hayo jana wakati wa kongamano la uwekezaji na ununuzi wa hisa na amana za Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (KCBL).

Alisema mali zote za vyama vya ushirika zilizochukuliwa bila kufuata utaratibu zitarudi kwenye mikono ya serikali.

Kusaya alisema mpaka sasa wamerejesha mikononi mwa serikali mali 59 za ushirika zilizochukuliwa bila kufuata utaratibu ambazo ni viwanja, nyumba, mitambo na vingine vyote vyenye thamani ya Sh. bilioni 68.9.

"Kama kuna mtu ana mali za ushirika kwa njia zisizo sahihi, azirudishe kwa hiari bila ya hivyo tuna nguvu nyingi za ziada haijalishi ziko wapi lazima tutazipata," alisema.

Kusaya alisema serikali itakuwa bega kwa bega na KCBL, ili kuhakikisha inaleta manufaa kwa Watanzania.

**Kama tunaamini katika ushirika lazima tuuheshimu na kulenga kufanya ushirika wa kibiashara katika kumkomboa Mtanzania tunataka kila mwanaushirika awe bilionea.**

"Kama tunaamini katika ushirika lazima tuuheshimu na kulenga kufanya ushirika wa kibiashara katika kumkomboa Mtanzania tunataka kila mwanaushirika awe bilionea," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya KCBL, Dk. Gervas Machimu, alisema benki hiyo iko imara kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi. Alisema wameshirikiana na Benki ya CRDB na wana bodi ya pamoja kwa lengo la kuboresha utendaji kazi.

Alisema serikali inayo ndoto ya kuendeleza viwanda na kutoa huduma katika kilimo na biashara na uwapo wa benki hiyo utasaidia kuendeleza sekta za uzalishaji na kusaidia zaidi ya asilimia 60 ya Watanzania wanaotegemea kilimo.

Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, alisema KCLB ni chama cha ushirika kilichoandikishwa kama benki na kimepata leseni ya kuhudumu kama benki ya ushirika kwa wananchi wa mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Tanga katika kilimo cha kahawa.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na CRDB, wamefanya jitihada ili benki isimame na kuhudumia makundi mbalimbali ya wakulima, wavuvi, wajasiriamali na wafugaji.

"Tukiamua leo kuikuza benki hii kwa kununua hisa tunaweza kuifikisha mbali. Vyama vikuu vya ushirika viko 46, lakini vinavyofanya kazi vizuri viko 30," alisema.

Alisema benki ya ushirika ya Kenya inafanya vizuri kutokana na uwekezaji uliofanyika na Tanzania ikiamua hakuna linaloshindikana.

"Kama tutafanya mabadiliko kwenye sekta ya kilimo, viwanda na uvuvi kama walivyofanya Kenya na kwenye benki ya ushirika wana uwekezaji ndio maana wamefanikiwa na benki yao ni ya tatu kwa ukubwa Kenya," alisema.

Mwenyekiti wa Kilimanjaro Development Forum (KDF), Dk. Abubakar Ibrahim, alitaka vyama vya ushirika kuchangamkia fursa ya uwekezaji kwenye vyama hivyo.




Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Kessy Maduka, akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani kimkoa katika viwanja vya Nyerere Square, jijini humo jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# SACCOS kutoa mikopo kukidhi mahitaji

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Rasilimali Watu na Utawala, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Victor Kategere, amekitaka Chama cha Akiba na Mikopo cha Mitaa kutoa mikopo kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya wanachama.

Wito huo aliutoa jana jijini hapa katika ufunguzi wa kikao cha chama hicho na kutaka wanachama kufanya urejeshaji wa mikopo kwa wakati na kuwa na ushiriki mzuri katika uchangiaji ili kusimama imara na kuwa msaada kwa wanachama wake.

"Na imani kila mwanachama anaelewa faida ya kujiunga katika chama chenu, hivyo basi mwendelee kuchangia na kushirikiana kwa karibu kwa kuweka na kukopa ili chama kidumu," alisisitiza Kategere.

Pia alisema wanachama hao wanatakiwa kufanya uhamasishaji mzuri kwa watu wengine ili kuongeza idadi ya wanachama na kufanya kuwa na idadi nzuri kusaidia kupata maendeleo zaidi.

Mwenyekiti wa chama hicho, Swedi Zidiheri, alisema kwa sasa bodi hiyo iko kwenye mchakato wa kufanya usajili kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

"Na hii ni kwa mujibu wa sheria mpya ya fedha inayotaka taasisi zote zinazohusika na masuala ya fedha zisajiliwe," alisema Zidiheri.

Zidiheri aliongeza kuwa wamefanikiwa katika kutoa mikopo kwa wanachama walioomba na kukidhi vigezo vilivyowekwa na hesabu za chama zimekaguliwa kuishia hadi mwaka 2019.

Pia alitoa shukrani kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhandisi Joseph Nyamhanga, ambaye ni mwajiri kwa kuwapatia ofisi kwa ajili ya shughuli za chama jambo ambalo limewapunguzia gharama za kulipia pango.



# Kapunga, Yala hali si shwari, silaha zatumika kulinda

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

HALI ya amani katika vijiji jirani vya Kapunga na Yala wilayani Mbarali, mkoani Mbeya sio shwari baada ya wakazi wa Kijiji cha Yala kuamua kulinda mashamba yao kwa kutumia silaha za jadi ili yasivamiwe na wenzao wa Kapunga.

Wananchi wa kijiji hicho ambacho kipo katika Kata ya Luhanga wamechukua uamuzi wa kulinda mashamba yao wakidai wenzao wa Kijiji cha Kapunga kilichopo Kata ya Itamboleo, wanavamia na kulima mashamba yao wakidai kuwa wamepewa na mwekezaji wa shamba la Kapunga Rice Project.

Wakizungumza na Nipashe kijijini hapo juzi, wananchi hao walisema kuwa kwa muda mrefu kumekuwapo na mgogoro wa ardhi baina ya mwekezaji na vijiji jirani na wao haukuwahi kuwahusu, lakini kwa sasa umeanza kuwahusu baada ya mwekezaji huyo kuanza kupanua mipaka ya shamba lake.

Mmoja wa wananchi hao, Manyanya Matabha, alisema baada ya mwekezaji kuanza kupanua mipaka, nyumba nyingi za wananchi wa kijiji chao hasa kitongoji cha Mwashikamile ziko hatarini kubomoka kutokana na kuzingirwa mara kwa mara na maji yanayotoka mashambani.

**Kitendo cha wananchi hao kuanza kulinda mipaka yao kwa kutumia silaha ni viashiria vya uvunjifu wa amani na kusisitiza kuwa atachukua hatua.**

Alisema pia wananchi hao kwa sasa wanaporwa mashamba, maeneo ya kuchungia na hivi karibuni walizuiwa kuendelea kujenga Shule ya Msingi Mwashikamile kwa madai kuwa ipo kwenye shamba la mwekezaji.

Alisema wamefikisha malalamiko yao kwenye ngazi mbalimbali za chama na serikali katika wilaya hiyo, lakini hawajapata msaada na kuamua kuanza kulinda mashamba yao dhidi ya wavamizi.

"Wananchi wameamua kuanza kulinda mashamba yao kwa kutumia sungusungu (vikundi vya ulinzi vya jadi) na juzi juzi hapa walitaka kuwashambulia baadhi ya watu wa Kapunga ambao waliokolewa na viongozi wa kijiji chetu waliowatuliza vijana hao," alisema Manyanya.

Naye Amos Mwanandi, alisema hawajawahi kushirikishwa na serikali wakati wa kuandaa shamba hilo na wanashangaa baadhi ya maeneo yao kudaiwa na mwekezaji kuwa yapo kwenye shamba la mwekezaji.

Alimwomba Rais Magufuli kuingilia kati mgogoro huo kwa maelezo kuwa viongozi wa ngazi ya wilaya wameshindwa kuutatua hali ambayo kwa sasa umeanza kuhatarisha amani baina yao.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Kata ya Itamboleo, Mohamed Kakwambi, alikiri kupokea malalamiko ya wananchi hao na kuyawasilisha kwa viongozi wa chama hicho ngazi ya wilaya na mkoa, lakini bado haujapata utatuzi.

Aliiomba serikali kusaidia kutatua mgogoro huo ikiwa ni pamoja na kuainisha vizuri mipaka ya shamba la mwekezaji ili kuondoa mwingiliano ambao unaweza ukasababisha maafa.

Akizungumzia mgogoro huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbarali ambaye ni Mkuu wa wilaya hiyo, Reuben Mfune, alisema eneo wanalolalamikia wananchi hao lipo ndani ya shamba la mwekezaji.

Alisema kitendo cha wananchi hao kuanza kulinda mipaka yao kwa kutumia silaha ni viashiria vya uvunjifu wa amani na kusisitiza kuwa atachukua hatua.

"Jambo hili halikubaliki na nilishatolea ufafanuzi mara nyingi na nilishawafafanulia kwa maandishi kuwa eneo hilo ni mali ya mwekezaji na ameweka utaratibu wa kuwagawia wananchi ili walime bure kabisa kwa kuomba," alisema Mfune.

Kijiji cha Yala ni miongoni mwa vijiji na vitongoji 21 vya Wilaya ya Mbarali ambavyo vilikuwa vinatakiwa kufutwa kwa madai kuwa vilikuwa vipo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.




Vijana wakitundika bango la kuwakumbusha madereva wa vyombo vya moto na watumiaji wengine wa barabara, kuzingatia alama za usalama barabarani katika eneo la Mafiati, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## UDSM yaomba eneo kujenga chuo Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), umeiomba Serikali ya Mkoa wa Mbeya kukisaidia chuo hicho kupata eneo lenye ukubwa wa ekari 500 kwa ajili ya kujenga chuo cha kisasa cha afya na sayansi shirikishi Mbeya pamoja na hospitali ya kufundishia wanafunzi.

Mkuu wa chuo hicho, Rais mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, alitoa ombi hilo juzi jijini Mbeya wakati wa mahafali ya 50 ya chuo hicho Ndaki ya Afya na Sayansi Shirikishi Mbeya (UDSM-MCHAS), ambayo yaliwahusisha wahitimu 223 wa udaktari wa binadamu.

Dk. Kikwete alisema kwa sasa chuo hicho kinatumia majengo ya Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya ambayo awali yalitakiwa yatumiwe na moja ya chuo kikuu kilichopo mkoani humo.

Alisema endapo chuo hicho kitapata eneo hilo kitaondoka ndani ya majengo ya hospitali hiyo na kwenda kujitegemea ili kuruhusu chuo kilichotakiwa kuyatumia awali kuendelea na mipango yake.

Awali, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo hicho, Mwanaidi Mtanda, aliishukuru Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kukisaidia chuo hicho majengo ndani ya hospitali hiyo pamoja na kuitumia hospitali hiyo kwa ajili ya mafunzo.

Alisema chuo pia kinawatumia madaktari wa hospitali hiyo kuwafundisha wanafunzi kwa nadharia na vitendo.

Alisema kutokana na upya wa Ndaki ya MCHAS, kuna matatizo mengi yameibuka ikiwamo kukosekana kwa makazi ya wafanyakazi, ofisi za wafanyakazi na malazi kwa ajili ya wanafunzi huku akieleza kuwa kwa sasa bodi kwa kushirikiana na uongozi wa chuo hicho unatafuta kiwanja.

Alisema endapo chuo hicho kitapata uwanja na kujenga mradi huo, utasaidia kuongeza hadhi ya Mkoa wa Mbeya pamoja na mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

# Asilimia 75 wanafunzi wanaumwa meno

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KATI ya asilimia 70 na 75 ya wanafunzi wa shule za msingi jijini Mbeya wanakabiliwa na matatizo ya kinywa na meno ikiwamo meno kutoboka na kuwauma.

Hayo yalibainika wakati wa wiki ya maadhimisho ya miaka 40 ya kuanzishwa kwa Chama cha Madaktari Bingwa wa Kinywa na Meno nchini (TDA), yaliyofanyika jijini hapa kwa madaktari hao kutoa matibabu bure kwa wananchi.

Madaktari hao wakishirikiana na madaktari bingwa wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, walitoa huduma ya matibabu bure ya kinywa na meno kwa wananchi katika Hospitali ya Kanda, viwanja vya Taasisi ya Uhasibu Mbeya (TIA) na kwenye shule mbalimbali za msingi.

Moja kati ya shule walizozitembelea ni Shule ya Msingi, Itiji iliyopo jijini Mbeya, Dk. Shamin Nasir, alisema idadi kubwa ya wanafunzi wa shule hiyo wana matatizo ya meno hasa kutoboka hali ambayo ni hatari kwa miaka ijayo.

"Kuna moja ya madarasa tumekuta darasa zima watoto meno yametoboka, sasa kuna kazi kubwa inayotakiwa kufanyika ikiwamo kuhamasisha watu kufanya usafi wa kinywa na meno kwa usahihi," alisema Dk. Shamin.

Naye Dk. Habiba Majapa, kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, alisema mbali na watoto hao kukabiliwa na tatizo la kutoboka kwa meno pia walibainii kuwa wengi wao wana mpangilio usio sahihi.

Aliwashauri wazazi na walezi kuwachunguza watoto wao meno mara kwa mara ili wakibaini kuwa yanatingishika yang'olewe katika muda mwafaka ili kuepuka kuota kwa kupandana na kusababisha mpangilio huo mbovu.

Alisema mpangilio mbovu wa meno unasababisha ugumu wa kusafisha meno kwa ufasaha kutokana na baadhi ya uchafu kushindwa kutoka kwa urahisi.





# Waziri aagiza uchunguzi wa mapato mabaraza manispaa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, ameiagiza Taasisi ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), kufanya uchunguzi wa makusanyo ya mapato na matumizi ya fedha katika mabaraza ya Manispaa ya Mkoa Mjini Magharibi.

Alisema katika kipindi cha wiki moja tangu aingie ofisini, alifanya ziara zake katika Manispaa ya Mjini, Magharibi A na Magharibi B Unguja na kutoridhishwa na utaratibu wa ukusanyaji wa mapato na matumizi yake katika manispaa hizo. Waziri Masoud aliyasema hayo jana katika mkutano wake na viongozi na watendaji wa mkoa, wilaya, jiji na mabaraza ya manipaa uliofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi, Vuga mjini hapa.

Alisema iwapo uchunguzi huo utabaini wapo waliohusika na vitendo vya ubadhirifu, serikali haitasita kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria bila ya kumwonea au kumnyanyasa mtu.

Alisisitiza kuwa serikali haiwezi kuacha vyombo vyake vya kukusanya mapato vikizembea katika suala la ukusanyaji wa kodi na kutumia fedha hizo bila kufuata utaratibu na mipango iliyowekwa.

"Nawataka wakurugenzi mkafanye upya tathmini juu ya makusanyo na matumizi ya fedha katika manispaa zenu, mimi nasema wazi siridhishwi na wala serikali hairidhishwi na utaratibu mnaoutumia kuna upotevu wa mapato ya serikali," alisema waziri huyo.

**Tunakoelekea na kwenda ni kufanya kazi kwa vitendo na uwajibikaji pamoja na kuchukua hatua badala ya kuhubiri maneno, serikali hii imepania kuwatumikia watu na kuwaletea maendeleo ili kuwajenga imani.**

Akizungumza na viongozi na watendaji hao, alisema haridhishwi na hali ya usafi wa mji na kuwataka wakurugenzi wa mabaraza ya manispaa kuanzia leo (Jumatano) hadi Jumapili kuanza usafi katika barabara ya mji na maeneo mbalimbali ndani ya mkoa huo. Masoud aliuagiza uongozi wa mkoa kusimamia usafi huo na kutafuta mbinu itakayokuwa endelevu ili kuhakikisha hali ya mji inakuwa safi wakati wote.

Kuhusu uwapo wa vikundi vya usafi katika mkoa huo, waziri huyo aliagiza kuvunjwa kwa vikundi visivyo na uwezo wa kufanya usafi na kuwataka kuingia mikataba mipya na vikundi vitakavyokuwa na tija na uwezo wa kufanya kazi hiyo.

Alisema kuwa serikali inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, imedhamiria kuwatumikia wananchi hivyo ni lazima viongozi na watendaji wawajibike ili umma uwe na imani juu ya utendaji wa serikali yao.

"Tunakoelekea na kwenda ni kufanya kazi kwa vitendo na uwajibikaji pamoja na kuchukua hatua badala ya kuhubiri maneno, serikali hii imepania kuwatumikia watu na kuwaletea maendeleo ili kuwajenga imani," alisema Masoud.

Katika mkutano huo waziri aliwataka wakurugenzi wa mabaraza ya manispaa na wasaidizi wao kutotumia muda mwingi kukaa ofisini na badala yake kwenda kwa wananchi kusikiliza kero zao na kuzipatia ufumbuzi.

Alisema kuwa dhana ya ugatuzi ni kuleta ufanisi katika utendaji ngazi ya serikali za mitaa, hivyo wana wajibu wa kuitendea haki dhamira hiyo ya serikali, na kutoa tahadhri kuwa hatasita kuchukua hatua kwa watendaji watakaoshindwa kuwajibika.

"Zipo changamoto zinazosababishwa na watendaji na hawachukui hatua, kila mmoja atimize wajibu wake katika nafasi yake na kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.

Wakati huo huo, Waziri Masoud aliuagiza uongozi wa mkoa kuzuia kufanywa biashara katika maeneo yasiyoruhusiwa na yasiyo rafiki ndani ya mkoa huo, ambayo imekuwa ikiharibu mandhari ya mji na hata kuleta changamoto serikali inapotaka kuwahamisha wafanyabiashara katika maeneo hayo.



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Muhammed Mussa (katikati), akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kikwajuni Zanzibar jana, wakati akitoa tathmini ya ziara yake ya wiki moja katika taasisi zilizochini ya wizara hiyo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Spika ataka Wawakilishi kuvaa nadhifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, amewataka wajumbe wa baraza hilo, kuwa nadhifu hasa katika suala la mavazi.

Aliyasema hayo juzi wakati akifunga semina ya wajumbe wa baraza hilo, Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar kuhusu uundwaji wa kamati za baraza.

Alisema miongoni mwa mambo yanayoweza kuharibu taswira ya wajumbe wa baraza hilo ni suala la mavazi wanayovaa wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Spika huyo alisema kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya watendaji na hata miongoni mwa wajumbe wa baraza hilo kuwa mavazi wanayovaa baadhi ya wajumbe hayaendani na hadhi zao.

"Katika Baraza la Wawakilishi lililopita yupo miongoni mwa waliokuwa wajumbe wa baraza hili alikuwa akija barazani anavaa malapa jambo ambalo halikubaliki," alisema.

Aliwataka wajumbe hayo kuwa wasafi na kuvaa mavazi mazuri ili kuendana na hadhi ya nafasi zao kwa sababu wao wanadhamana kubwa kwa umma.

Aliwataka wajumbe hao kuwa kioo kwa jamii inayowawakilisha, hivyo ni vyema kuwa na heshima ambayo inaanza kupimwa katika mavazi.

"Kitendo cha kuvaa mavazi yasiyoendana na hadhi yetu wakati wa kazi za kamati kama vile fulana na nguo nyingine zenye kushusha hadhi yetu, zinazifanya kamati zetu zidharauliwe mbele ya watendaji tunaowasimamia," alisema Spika Zuberi.

Kadhalika, alisema suala la mavazi limekuwa likijitokeza wakati wa vikao vya Baraza la Wawakilishi kwa baadhi ya wajumbe kuvaa mavazi yanayokwenda kinyume na kanuni.

Alisema ni vyema wakajirekebisha katika suala la mavazi yenye hadhi na heshima ili kutunza hadhi na heshima.

**Katika Baraza la Wawakilishi lililopita yupo miongoni mwa waliokuwa wajumbe wa baraza hili alikuwa akija barazani anavaa malapa jambo ambalo halikubaliki.**

# Zaidi ya tani 100 mchele basmati zateketezwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya tani 112 za mchele aina ya basmati zimeteketezwa baada ya kupitwa na muda wa matumizi ili kuwanusuru afya za watumiaji.

Tani hizo zimeteketezwa katika Jaa la Kibele Wilaya ya Kati Unguja baada ya kufanyiwa uchunguzi na kugundulika kuwa umepitwa na muda kwa matumizi ya binadamu.

Mkurugenzi wa Idara ya Udhibiti wa Usalama wa Chakula Zanzibar (ZFDA), Dk. Khamis Ali Omar, alisema wakati akitoa maelezo kwa waandishi wa habari kuhusu kuteketezwa kwa tani hizo.

Alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara wanafanya udanganyifu wa kuzibadilisha bidhaa zilizokwisha muda wa matumizi na kuziingiza katika vifungashio vipya jambo ambalo linahatarisha afya ya watumiaji.

Alisema kuwa mchele huo umegundulika katika ghala la Akhtar enterprises (maarufu Simba Chai) liliopo Mombasa Unguja na kukutwa idadi kubwa ya vipolo (viroba) vitupu vilivyobadilishwa tarehe na mwaka kwa ajili ya kufungwa tena mchele huo ili uendelee kutumika.

Dk. Khamis alisema kuwa pia wamegundua tambi ambazo zimepitwa na wakati pamoja na vifuko vitupu vilivyobadilishwa mwaka kwa ajili ya kuzifunga upya ili kuanza kusambazwa katika maduka mbalimbali kwa ajili ya matumizi.

Hata hivyo, mkurugenzi huyo alisema kwa sasa mmiliki wa ghala hilo ameshafikishwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

Naye Mkuu wa Ukaguzi wa Chakula (ZFDA), Suleiman Akida Ramadhan, aliwataka wananchi kuangalia na kuzichunguza kwa makini wakati wanaponunua bidhaa mbalimbali na wakigundua kuna hitilafu yoyote watoe taarifa kwa mamlaka zinazohusika.

Alisema ZFDA itahakikisha inaendelea kufanya ukaguzi wa bidhaa zilizopo sokoni ili kuziondoa zilizopita muda wa matumizi ya binadamu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**

Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**


NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**JALFA AHMADI** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S1394/0103** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA SHULE YA SECONDARY KATORO ISLAMIC SEMINARY MWAKA 2014,YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**POLISI TAARIFA**
**DAR/MSI/RB/829831/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FATUMA RASHIDI** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S0338/0012** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA SHULE YA SECONDARY NDANDA MWAKA **2002,**YEYOTE ATAKAYEKIOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**POLISI TAARIFA**
**DAR/URA/RB/831291/2020**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SINGANO RAMADHANI** DANGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S.155/94** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA TABORA BOYS SEKONDARI MWAKA **1976**. YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

**TAARIFA YA POLISI:**
**KOR/RB/2559/2020.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**NURU JOHN NZIKU** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA VYETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S.4549/0055** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA SHULE YA SECONDARY LUGANGA MWAKA **2017,**RESULT SLIP YA KIDATO CHA SITA INDEX NAMBA **S.2191/0537** SHULE YA MWANAMEMA SHEIN MWAKA 2020,YEYOTE ATAKAYEVIOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**POLISI TAARIFA**
**DAR/CHU/RB/831623/2020**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**LUCAS MOTURA NYAKURATA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HONDA** yenye namba za usajili **MC 455 BAP.Chassis No LWAPCJL607A891195**, Engine **No.156FMIX7A607170A.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi**
**DOD /DOD/RB/285706/2020.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GIDION NHONYA MASAGASI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TOYO** yenye namba za usajili **MC 917 BDP.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**
**URP /RB/297/19.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**CLAUDIA ONESMO ALBERT** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA VYETI , CHA KIDATO CHA NNE INDEX NAMBA **S 0557-0003** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA SHULE YA SECONDARY NARUMU MWAKA 2011,CHETI CHA KIDATO CHA SITA INDEX NAMBA **S 0255-0520** SHULE YA ST.CHRISTINA SECONDARY MWAKA **2014,**PAMOJA NA CHETI CHA JESHI JKT **823** MSANGI,PAMOJA NA CHETI CHA KUZALIWA.

**POLISI TAARIFA**
**DAR/MAG/RB/78043/2020**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**SUZAN KENNETH WOISO** ANATANGAZA KUPOTEA KWA RESULT SLIP YA KIDATO CHA SITA YENYE INDEX NAMBA **S.0248-0661** ILIYOTOLEWA NA MARIAN GIRL'S SEKONDARI MWAKA **2020.**

**YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.**
**CONTROL NO: 9910819818001.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NANCY JULIUS KALLAMBO** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba za usajili **T 550 DMH** chasis namba **NCP600058032**,yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa DOD/DOD/RB/830161/2020**

## REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT

(CAP 117)

CHANGE OF NAME BY DEED POLL

**THIS CHANGE OF NAME DEED** is made this 18th day of November, 2020 by me **FOCUS JOSEPHAT NTAKAMLENGA** formerly known as **FOCUS JOSEPHAT of P.O. Box SONGEA,** now or until recently called **FOCUS JOSEPHAT KITTUMBU. WITNESSES AND IT IS HEREBY DECLARED** as follows: I absolutely renounce and abandon the use of my said name of **FOCUS JOSEPHAT AND FOCUS JOSEPHAT KITTUMBU AND FOCUS JOSEPHATI** and I assume and determine to take and use the name of **FOCUS JOSEPHAT NTAKAMLENGA** in substitution of my name of **FOCUS JOSEPHAT AND FOCUS JOSEPHAT KITTUMBU AND FOCUS JOSEPHATI. AND IN PURSUANCE** of such change of name(s) as aforesaid **I DECLARE**, I shall at all times hereafter in all records, documents and other writings and in all actions and dealings and on all occasions whatsoever use the name **of FOCUS JOSEPHAT NTAKAMLENGA** in substitution for my names of **FOCUS JOSEPHAT AND FOCUS JOSEPHAT KITTUMBU AND FOCUS JOSEPHATI** so relinquished as aforesaid to the intent that I may hereafter be known not by the aforesaid name, but by the name of **FOCUS JOSEPHAT NTAKAMLENGA** only.

**AND I HEREBY AUTHORISE AND REQUIRE** all persons at all times to describe and address me by the name of **FOCUS JOSEPHAT NTAKAMLENGA. IN WITNESS FOCUS JOSEPHAT NTAKAMLENGA** whereof I have hereunto subscribed name of **FOCUS JOSEPHAT NTAKAMLENGA** and have affixed my signature the day and year herein written.

**SIGNED and DELIVERED by the said FOCUS JOSEPHAT NTAKAMLENGA** who is introduced to me personally in my presence this **18th day of November, 2020.**







OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
MOB:
+255 - 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA

# Wizara yawashukia wasioendeleza viwanja

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imewaonya wamiliki wote wa ardhi wenye viwanja visivyoendelezwa na kulipiwa kodi ya pango na kuwataka kulipa ndani ya siku 14, vinginevyo watanyang'anywa.

Mkuu wa Kitengo cha Kodi katika wizara, Denis Masami, alisema hayo wakati wa kuhamasisha ulipaji kodi ya pango la ardhi katika mtaa wa Chidachi jijini Dodoma ikiwa ni mkakati wa wizara kuhakikisha wamiliki wote wa ardhi wanalipa kodi ya pango kwa wakati.

Alisema wizara kupitia ofisi zake za ardhi za mikoa, imeanzisha utaratibu wa kuwatembelea wamiliki wa ardhi kila mwisho wa wiki kwa lengo la kuhamasisha ulipaji kodi na kutoa elimu, ili kuwawezesha kutekeleza jukumu hilo bila shuruti.

"Maeneo mengi nchini yana viwanja visivyoendelezwa na wakati huo wamiliki wake hawavilipii kodi ya pango la ardhi jambo linaikosesha mapato serikali. Baada ya siku 14 tutaanza utaratibu wa kuvitwaa na kuvinadi ili kufidia deni na kumilikishwa kwa watu wengine," alisema Masami.

Alisema wizara inatekeleza mkakati wake wa kuhamasisha ukusanyaji kodi ya pango la ardhi kwa kushirikisha wataalamu wa sekta ya ardhi na makamishna wasaidizi wa ardhi katika mikoa kwa kupita nyumba kwa nyumba na kuwapelekea wadaiwa ankara za madai ya ulipaji kodi ya pango la ardhi na maduhuli mengine yatokanayo na sekta ya ardhi ili kulipa.

Akiwa eneo la Chidachi, Masami alibaini maeneo kadhaa yasiyoendelezwa na wamiliki wake kudaiwa kodi ya pango la ardhi sambamba na ukubwa wa eneo la Shule ya St. Mary's Dodoma kuonyesha kuwa na ukubwa wa Square mita 900 wakati uhalisia ni hekta 3.5, jambo alilolieleza kuwa limeifanya shule hiyo kulipia kiasi kidogo cha kodi ya pango la ardhi.

Ofisa Ardhi wa Jiji la Dodoma, Ruta Rwechugura, alisema wakati wa kuwafuatilia wadaiwa wa kodi ya pango la ardhi, walibaini kukiukwa kwa baadhi ya taratibu na wamiliki wa ardhi na kutolea mfano ubadilishaji matumizi ya umiliki sambamba na baadhi ya wananchi kuuziana viwanja bila kubadilisha jina.

Aliwataka wamiliki wote wa ardhi walionunua viwanja kwenye maeneo mbalimbali nchini kuhakikisha wanabadilisha umiliki kwa kufika ofisi za ardhi katika halmashauri husika, ili kuiweka ardhi yao salama na kuwasisitizia wamiliki kutobadili matumizi ya viwanja bila kufuata taratibu.

Mmoja wa wananchi waliofikiwa na maofisa hao, Faustine Mwakalinga, alipongeza wizara kwa uamuzi wake wa kuwafikia wamiliki wa ardhi kwa lengo la kutoa elimu na kuhamasisha ulipaji kodi ya ardhi.

Alisema utaratibu huo unapaswa kuigwa na watendaji wengine wa serikali katika kudai kodi kwa kuwa ni utaratibu rafiki na unamhamasisha mdaiwa kulipa badala ya kuogopa.

# Wafunguliwa mashtaka 28 ya rushwa, kughushi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma kwa kushirikiana na Ofisi ya Mashtaka ya Taifa, imewafikisha katika Mahakama ya Hakimu Mkazi watu wanne na kuwafungulia mashauri mawili yenye jumla ya mashtaka 28 yanayohusu vitendo vya rushwa na kughushi.

Aidha, TAKUKURU imeokoa Sh. milioni 11.9 ambazo zilikuwa zinalipwa katika akaunti ya benki ya mtumishi marehemu kama mshahara kuanzia Oktoba 2013 hadi Machi 2016 kinyume cha utaratibu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema shauri la kwanza la jinai linamkabili Aithan Chaula (61) aliyekuwa Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Chamwino na mratibu wa pembejeo za kilimo za ruzuku kwa msimu wa 2015/16. Mtuhumiwa mwingine ni Michael Mpembwa (44) ambaye ni Mkurugenzi wa kampuni ya Agro Suppy iliopewa uwakala wa kusambaza pembejeo za kilimo katika kijiji cha Zajilwa kilichopo wilayani Chamwino mkoani hapa.

Kibwengo alisema watuhumiwa hao watashtakiwa kwa makosa 25 ya kughushi kinyume na sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16.

Alifafanua kuwa uchunguzi unaonyesha kwamba kati ya Januari na Agosti 2016, watuhumiwa hao walighushi nyaraka ambazo zilionyesha kwamba wakala alisambaza pembejeo zikiwamo mbegu za mahindi na mbolea kwa wakulima wa Zajilwa na hivyo kulipwa Sh. milioni 14 wakati wakifahamu kwamba ni uongo.

Alisema kosa hilo ni kinyume na Kifungu cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007 na sheria nyinginezo.

Akitolea ufafanuzi kuhusiana na fedha za mshahara wa mtumishi marehemu alisema TAKUKURU inaendelea kufuatilia ili kubaini kitendo hicho kilifanywa na watu gani ili wachukuliwe hatua stahiki za kisheria.

Hata hivyo, Kibwengo aliwataka watumishi wa umma na jamii nyingine kutambua kuwa rushwa ni kosa la jinai na huwa haifi, hivyo wahakikishe wanakwenda kulingana na sheria, kanuni na taratibu za nchi.

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'**


SIMU NA :027-2530022
2530042
FAX NA :027/ 2530022
:027/ 2530042

Ofisi ya Mkurugenzi
Mtendaji (W),
S.L.P. 2,
KATESH-HANANG'
MANYARA.
30/11/2020

Baruapepe:ded@hanangdc.go.tz
Tovuti: www.hanangdc.go.tz


## TANGAZO LA ZABUNI
## TANGAZO LA ZABUNI YA KUKUSANYA USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI

**ZABUNI NA.LGA/059/2020-2021/NC/11**

Halmashauri ya Wilaya ya Hanang inawatangazia wananchi wote, Makampuni au watu Binafsi wenye sifa kuomba Zabuni ya Uwakala wa kukusanya Ushuru wa nyumba za kulala wageni katika Halmashauri kwa mwaka 2020/2021.

| S/N | CHANZO | NA. YA ZABUNI |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa Nyumba za kulala wageni | LGA/059/2020-2021/NC/11. |

1. LGA/059/2020-2021/11
- Ushuru wa nyumba za kulala wageni itahusu kukusanya ushuru wa nyumba zote za kulala wageni katika halmashauri ya wilaya ya Hanang'.

MASHARTI YA ZABUNI:

Barua za maombi ziambatanishwe na maelezo kamili na vivuli vya nyaraka zilizothibitishwa zifuatazo;-

1. Mwombaji lazima awe na leseni hai ya Biashara ya uwakala wa kukusanya mapato, awe na TIN, VAT kwa waliosajiliwa, awe na Kampuni iliyosajiliwa na BRELA au jina la biashara lililosajiliwa na
2. BRELA (Business Name) na uthibitisho ulipaji kodi(Tax clearance Certificate) ya mwaka 2020.
3. Mwombaji anatakiwa kununua kabrasha la Zabuni (Tender Document) baada ya kulipa ada ya maombi ya Zabuni isiyorudishwa ya Tshs 100,000.00. Fedha hizo zilipwe kupitia benki/wakala baada ya muombaji kupewa Bili na Mhasibu wa Halmashauri ya Wilaya siku za kazi yaani Jumatatu – Ijumaa kuanzia saa 1:30 Asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri na Nyaraka za Zabuni zinapatikana kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya.
4. Mwombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kuhakikisha kuwa anakusanya taarifa za nyumba za kulala wageni kwa kila siku na kuwasilisha taarifa kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya kwa ajili ya kuandaa hati ya madai na mzabuni atarudishiwa "Commission" isiyozidi asilimia ishirini (20%) kulingana na makusanyo kwa mwezi.
5. Mwombaji aambatanishe maelezo ya kazi alizowahi kuzifanya, uzoefu usiopungua miaka miwili
6. Mwombaji alete orodha ya majina ya wenye Kampuni au Wakurugenzi wenye hisa za Kampuni au mmiliki wa Biashara pia idadi ya wafanyakazi, ujuzi na uzoefu.
7. Mwombaji wa zabuni awasilishe nyaraka za uwezo wa kifedha" Bank statement" za miezi mitatu.
8. Mwombaji aambatanishe uhalali wa kisheria wa mtu atakayehusika na Zabuni (Power of Attorney)
9. Mwombaji asiwe Mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang (A Public Officer) au Mheshimiwa Diwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'.
10. Mwombaji atakayefanikiwa Zabuni hii atatakiwa kuilipa Halmashauri malipo ya miezi mitatu (3) kabla hajaanza kukusanya mapato kama dhamana ya utendaji kazi. Dhamana inaweza kuwa fedha taslim au Dhamana ya Benki (Bank Guarantee) sawa na Fedha za malipo ya miezi mitatu ambayo muombaji ataweka kwenye Zabuni yake. Dhamana itawasilishwa baada ya muombaji kujulishwa ushindi wake.
11. Mwombaji atakayefanikiwa kuwa Mzabuni atakusanya ushuru kulingana na viwango vilivyowekwa na Halmashauri pamoja na Sheria Ndogo za Halmashauri (By-Laws).
12. Maombi yote ya Zabuni yakiwa katika kabrasha halisi moja na nakala mbili (1 original and 2 copies) yawekwe ndani ya bahasha isiyo na maandishi (Plain envelope) yafungwe kwa lakiri juu ya Bahasha iandikwe ZABUNI NA.LGA/059/2020-2021/NC/11
13. Maombi yatumwe kwa :-

**KATIBU WA BODI,**
**BODI YA ZABUNI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG'**
**S.L.P 2, KATESH – HANANG'.**

14. Mwisho kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 11/12/2020 ya saa 5.00 Asubuhi katika Ofisi ya Manunuzi Halmashauri ya Wilaya, Block A, Chumba Na.18 na Zabuni zitafunguliwa baada ya muda wa mwisho wa kuleta Zabuni.
15. Maombi ambayo hayatapokelewa na kusomwa siku ya ufunguzi hayatakubaliwa.
16. Waombaji wa zabuni au wawakilishi wanakaribishwa siku ya ufunguzi.

**SOLOMON I. SHATI**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HANANG'**



# LOW KUENDELEA KUPETA UJERUMANI

**MUNICH,** Ujerumani

JOACHIM Low ataendelea kuwa Kocha Mkuu wa Ujerumani baada ya majaliwa yake kuhojiwa kutokana na kichapo cha mabao 6-0 dhidi ya Hispania.

Presha ilikuwa kubwa kwa mshindi huyo wa Kombe la Dunia baada ya kufanywa vibaya kwenye Ligi ya Mataifa ya Ulaya mapema mwezi uliopita na Chama cha Soka cha Ujerumani (DFB), kilisema kutakuwa na muda wa kuangalia hali hiyo.

Juzi, Jumatatu DFB ilithibitisha kwamba kinamsapoti kwa asilimia zote kocha huyo mwenye umri wa miaka 60 na kukanusha uvumi kuhusu hatima yake.

Taarifa hiyo ya DFB ilikuja baada ya uvumi kuzagaa kwamba Low, ambaye yupo kwenye nafasi hiyo tangu mwaka 2006, ataachia ngazi muda wowote pamoja na Mkurugenzi wa timu ya Taifa, Oliver Bierhoff.

"Lilikuwa jambo muhimu kwa kocha wa timu ya taifa kujadili hali ya sasa, kipigo kutoka kwa Hispania kimetoa muda mzuri wa kukifanyia kazi kikosi," ilisomeka taarifa ya DFB.

Kazi kubwa aliyonayo sasa Low ni kukiimarisha kikosi hicho kwenye michuano ya Euro 2020 inayofanyika mwakani.

# Klopp aelezea hali ya Van Dijk

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema Virgil Van Dijk anaendelea vizuri na kwamba, anaonekana anaweza kupona haraka zaidi.

Van Dijk aliumia goti mwezi uliopita kwenye mchezo dhidi ya Everton baada ya kugongana na golikipa, Jordan Pickford.

Nyota huyo wa kimataifa wa Uholanzi, anaweza kukosa michuano ya Euro 2020 ambayo ilisogezwa mbele na inatarajiwa kufanyika mwakani.

Kukosekana kwake kumeonekana pigo kubwa kwa 'Wekundu' hao ambao aliwasaidia kutwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu England kwa kipindi cha miaka 30, msimu uliopita.

Van Dijk alicheza pasi 3,255 zikiwa nyingi zaidi kuliko mlinzi yeyote wa Ligi Kuu England.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, alifanyiwa operesheni mwishoni mwa Oktoba, huku Klopp akithibitisha kwamba anaendelea vizuri.

Alipoulizwa kama anawasiliana mara kwa mara na Van Dijk, Klopp aliviambia vyombo vya habari: "Ndio, bila shaka tunawasiliana. Na anaendelea vizuri sana.

"Goti lake haliko vizuri kwa kweli. Lakini naamini anaweza kupona haraka tu.






# Barca kuchagua rais wao Januari

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imetangaza kwamba watafanya uchaguzi wa urais Januari 24, mwakani.

Rais wa sasa, Josep Maria Bartomeu (pichani) na bodi yake walijiuzulu Oktoba siku chache kabla ya kupigiwa kura ya kutokuwa na imani.

Rais wa zamani, Joan Laporta, alitangaza mapema Jumatatu kwamba atagombea urais, akielezea kutaka kurudi kwake kwenye nafasi hiyo kama "changamoto kubwa kwenye maisha yangu ".

Wagombe wengine wanaotarajiwa kuwania urais ni Jordi Farre, Toni Freixa, Lluis Fernandez Ala, Agusti Benedito, Pere Riera na Victor Font, ambaye anapewa nafasi kubwa.

Makamu wa Marais wa zamani, Emili Rousaud na Girona, Mkurugenzi wa zamani, Xavi Vilajoana na Jordi Roche pia wanatajwa kuwania nafasi hiyo.

Barca ilithibitisha Jumatatu kwamba, kampeni kwa ajili ya uchaguzi huo itafanyika Januari 15 hadi 22 kabla ya uchaguzi kufanyika.

# Jimenez azungumza baada ya operesheni

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Wolves, Raul Jimenez amezungumza kwa mara ya kwanza kupitia twitter baada ya kufanyiwa upasuaji kutokana na mshtuko kwenye ubongo.

Raia huyo wa Mexico amezungumza kwa mara ya kwanza baada ya kufanyiwa upasuaji kwa kuwa alipata mshtuko alipogongana na David Luiz kwenye mchezo wa Ligi Kuu Engand Jumapili, ambapo Arsenal ilipoteza kwa kufungwa mabao 2-1.

Nyota huyo amesema bado yupo kwenye matibabu na anaamini kwamba atarejea uwanjani hivi karibuni kwa kuwa anaendelea vizuri.

Jimenez ameweka wazi kuwa shukrani zake ni kwa Mungu pamoja na mashabiki ambao wamekuwa wakimtumia ujumbe kwa ajili ya kumjulia hali na kumwombea kheri.

"Asante kwa sapoti kupitia meseji zenu mashabiki, nipo kwenye maendeleo mazuri kwa sasa na nina matumaini kwamba nitarejea uwanjani hivi karibuni," alisema.





# CAVANI APAMBANA KUJITETEA KUFUNGIWA

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United, Edinson Cavani, ameomba radhi na kufuta posti yake ambayo alikuwa ameiweka kwenye mitandao yake ya kijamii ambayo ilikuwa na ujumbe uliohusishwa na vitendo vya kibaguzi katika baadhi ya mazingira.

Mshambuliaji huyo raia wa Uruguay alitokea benchi na kuisaidia klabu ya Man United kuondoka kifua mbele akifunga mabao mawili katika ushindi wa 3-2 dhidi ya Southampton kwenye Ligi Kuu England.

Tayari Chama cha Soka England kimesema kinaendelea kufuatilia ujumbe huo uliokuwa kwa lugha ya Kihispania. "Nilikuwa nakusudia kuwasalimia ndugu zangu, na kuwashukuru kwa kunipa moyo wa kila siku kupambana," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33.

"Napingana kabisa na ubaguzi wa rangi, nilifuta ujumbe ule baada ya kuambiwa kuwa unaweza kuchukuliwa tofauti na watu wengine kwenye maeneo mengine pia."

United wanajua kuhusiana na hilo na wametafsiri vile ambavyo Cavani alikuwa anakusudia.

Taratibu za FA zinasema mchezaji yeyote atakayebainika kuwa na makosa ya ubaguzi wa rangi atafungiwa angalau kwa mechi tatu.

# *Sababu daktari wa Maradona kuchunguzwa*

**BUENOS AIRES,** Argentina

WAENDESHA mashtaka nchini Argentina wanamchunguza daktari wa Diego Maradona, Leopoldo Luque (pichani), wakimshuku kwa kuhusika na kifo cha nyota huyo wa soka kilichotokea Novemba 25, mwaka huu.

Polisi mjini Buenos Aires wameisaka nyumba na kliniki ya daktari huyo huku wakijaribu kubaini iwapo ulikuwapo uzembe katika matibabu baada ya upasuaji aliofanyiwa Maradona.

Maradona ambaye alikuwa na umri wa miaka 60, alifariki dunia kutokana na shinikizo la damu nyumbani kwake ambako alikuwa akiendelea kupona baada ya kufanyiwa upasuaji.

Polisi wanashuku kwamba nyota huyo wa soka aliruhusiwa kwenda nyumbani kwake akiwa bado hajatimiza masharti ya kumruhusu atoke hospitalini, ikiwamo kupewa wauguzi au nesi wa kumhudumia saa 24, wataalamu wa uraibu, kupewa daktari anayeweza kumuita wakati wowote na gari la kubebea wagonjwa lenye vifaa vya kumsaidia kupumua.

Maofisa wanataka kufahamu kuhusu uhusika wa daktari Luque katika mipango ya kupona kwa Maradona katika nyumba ya nyota huyo.

Maradona alifanyiwa upasuaji kwenye mshipa wa ubongo kutokana na kuganda kwa damu, ambapo mapema Novemba alikuwa akipata matibabu kutokana na uraibu wa pombe.

Familia ya Maradona inafuatilia kwa makini sakata hilo ili kubaini kama daktari huyo alifanya uzembe wakati wa upasuaji.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD ANA WAKATI MGUMU MNO - ZIDANE

### Ni hali ambayo inamchanganya Eden, hajawahi kuwa majeruhi kwa kipindi kirefu...

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane anatambua kwamba, Eden Hazard anapitia "wakati mgumu" lakini amesisitiza Real Madrid watafanya kila kitu wanachoweza kumsaidia mchezaji huyo waliyemsajili kwa ada iliyoweka rekodi.

**Nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amekuwa na matatizo ya muda mrefu ya kifundo cha mguu na matatizo ya mguu tangu alipojiunga na miamba hao wa Hispania kutoka Chelsea karibia miezi 18 iliyopita.**

Msimu uliopita alianza katika mechi 14 za LaLiga, akiwa hana mchango mkubwa wakati Madrid wakitwaa taji la Ligi Kuu.

Ameendelea kuwa kwenye wakati mgumu msimu huu na aliumia tena kwenye mchezo wa Jumamosi wa kichapo kutoka kwa Deportivo Alaves.

Hakuna muda uliowekwa kuhusu kurudi kwake na hakutajwa kwenye kikosi cha Madrid kilichoshuka dimbani jana Jumanne kucheza na Shakhtar Donetsk kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Zidane amesema Madrid ina jukumu la kumwangalia na kumfuatilia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, na anaamini straika huyo atarudi kwenye kiwango chake na kuwa imara zaidi.

Alipoulizwa na waandishi wa habari kama Hazard anapitia wakati mgumu zaidi kisaikolojia kutokana na majeraha hayo, Zidane alijibu: "Hapana. Kuna wakati majeraha yanatokea na tunatakiwa kuwa wavumilivu. Yeye ni imara, sina shaka na hilo.

"Ana wakati mgumu kwa sasa. Tutamsaidia kuwa bora zaidi.

"Ni hali ambayo inamchanganya Eden. Hajawahi kuwa majeruhi kwa kipindi kirefu kama hiki na pengine ni bahati mbaya tu.

"Nina uhakika atarudi na kuwa imara kama mwanzo. Tunamtarajia kuwa bora na kuimarika zaidi na sisi."

## ZISIKUPITE

### GIROUD ATAKIWA INTER

INTER Milan inataka kumsajili mshambuliaji wa Chelsea, Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34, kwa mkopo wa miezi sita Januari, huku kukiwa na kipengele cha kumnunua jumla. ***(Tuttosport via Mail)***

### JUVE YAJITOSA KWA GIROUD

INTER Milan inakabiliwa na ushindani mkubwa kwenye mbio za kumwania Olivier Giroud mwenye miaka 34 kutoka Chelsea, kutoka kwa Juventus ambapo kocha wake, Andrea Pirlo anataka kumsajili wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Ilbianconero via Calciomercato)***

### CHELSEA WAMTAKA ALABA

CHELSEA itafungua mazungumzo na Bayern Munich kuhusu mlinzi David Alaba mwenye umri wa miaka 28, baada ya kutaka kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Austria akiwa huru mara tu mkataba wake utakapomalizika kipindi cha majira ya joto kijacho. ***(AS via Sun)***

### UNITED YAMWANIA TORRES

MANCHESTER United ina matumaini Villarreal inaweza kujaribu kumchukua mlinzi wake wa zamani, Eric Bailly mwenye umri wa miaka 26 raia wa Ivory Coast, kama sehemu ya kumwachia mlinzi wake wa kati Pau Torres mwenye umri wa miaka 23 ambaye thamani yake inatajwa kuwa ni pauni milioni 60. ***(Team Talk)***

### LIVER KUMSAJILI SCHUURS

LIVERPOOL inataka kumsajili mlinzi wa Ajax, Perr Schuurs, kwa ada ya pauni milioni 27 ili kumchukua nyota huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(De Telegraaf)***

### SPURS YAMWANIA FERRARI

KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia mlinzi wa kati wa Sassuolo, Gian Marco Ferrari mwenye umri wa miaka 28, ili wamsajili wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(90min)***

### ERIKSEN ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United inaweza kumsajili kiungo wa Inter Milan, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 28, kama raia huyo wa Denmark hatatakiwa na klabu yake ya zamani, Tottenham. ***(Football Insider)***

### MESSI ALIVYOGOMEWA INTER

BARCELONA ilikataa ofa ya pauni milioni 224 kutoka kwa Inter Milan kwa ajili ya kumuuza nyota wake wa kimataifa wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, mwaka 2006, kwa mujibu wa Rais wa zamani, Joan Laporta. ***(Football Italia)***

### MARTINEZ KUIACHA BAYERN

KIUNGO wa Bayern Munich, Javi Martinez mwenye umri wa miaka 32, amedokeza ataondoka kwa miamba hao wa Ujerumani mara tu mkataba wake utakapomalizika Juni mwakani. ***(Reuters via Eurosport)***

## TBS wapongezwa viwango SHIMMUTA

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI wa timu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) walioshiriki mashindano ya Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma na Makampuni Binafsi Tanzania (SHIMMUTA) mkoani Tanga, wamepongezwa kwa kuonyesha viwango vya juu michezoni wakati wakishiriki michuano hiyo na kufanikiwa kutwaa mataji.

Pongezi hizo zilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Upimaji na Ugezi wa TBS, Johanes Maganga wakati akizungumza na wachezaji wa shirika hilo walioshiriki mashindano hayo yaliyomalizika mwishoni mwa wiki.

Huku akitoa wito kwa wachezaji wa shirika hilo kuendelea kufanya mazoezi ili kujiandaa kwa mashindano yajayo, alieleza kuridhishwa na jinsi wachezaji walivyojituma kwenye mwaka huu kwenye mashindano hayo yaliyokuwa na ushindani mkubwa.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Mkuu wa TBS, Dk. Yusuf Ngenya, alisema shirika hilo limeshiriki mashindano hayo kwa miaka sita mfululizo na kwamba kushiriki michezo hiyo kuna maana nyingi.

"Kwanza michezo inaleta afya na inasaidia kuleta ufanisi, kwani katika kazi zao za kila siku zinakwenda vizuri, hivyo na ufanisi unapatikana vizuri," alisema Dk. Ngenya na kuongeza;

"Mashindano hayo yana umuhimu kwani zaidi ya afya yanawaweka pamoja na hiyo haishii kwenye michezo bali kuleta utendaji wa pamoja."

Katika mashindano hayo wachezaji wa timu ya TBS walitwaa baadhi ya mataji, ambapo kwenye mashindano ya kufuta kamba timu ya wanaume ilishika nafasi ya tatu. Kwa upande wa mpira wa pete wanaume katika kundi lake TBS ilikuwa na timu nne kutoka SUA, DUCE, TANESCO. Katika michezo yake, TBS iliifunga SUA seti 2-0, wakaifunga DUCE seti 2-0, hivyo kuingia robo fainali.

Katika mchezo wa robo fainali walitolewa kwenye mashindano hayo baada ya kufungwa na timu ya Mamlaka ya Wanyama Pori Ngorongoro.

Katika mchezo wa drafti kwa wanawake timu hiyo iliibuka mshindi wa tatu baada kuichapa Muhimbili huku katika mppira wa pete kwa wanawake kwenye hatua za makundi, TBS ilikuwa kundi moja na timu za Mbeya-AUWASA, TMDA, SUA,NHIF na TANESCO.

# GRR YAZINDUA GOBA HILLS MARATHON 2021

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Goba Roads Runners (GRR), imezindua rasmi msimu wa pili wa mbio za Goba Hills Marathon, zinazotarajiwa kufanyika Januari 30, mwakani kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Goba, Ubungo jijini Dar es Salaam.

**Lengo kuu la mbio hizo imeelezwa kuwa ni kuboresha afya ya mama na mtoto kwa kuboresha mazingira ya hospitali hasusan wodi za kujifungulia.**

Baada ya mbio hizo kufanyika kwa mafanikio makubwa msimu wa kwanza Februari mwaka huu, msimu huu wa pili wa Goba Hills Marathon 2021, unakwenda kwa kaulimbiu ya "Kimbia, Okoa Maisha ya Mama na Mtoto".

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Goba Hills Marathon , Benson Luoga, alisema mbio hizo zitakuwa za Kilomita 42.2 (Full Marathon), Kilomita 21.1 (Half Marathon), Kilomita 10 (Corporate Run) na Kilomita tano (Family Run).

Luoga alisema usajili kwa ajili ya kushiriki mbio hizo ni Sh. 30,000 kwa kila mbio na tayari umeshafunguliwa na washiriki wameanza kujisajili kupitia tovuti ya club ya GRR ambayo ni www.grr.co.tz.

"Katika mbio za msimu wa kwanza, sehemu ya mapato yaliyopatikana yalitumika kununua vifaa vichache vya kumsaidia mama na mtoto wakati wa kujifungua pamoja na kuweka mfumo wa umeme jua (solar system) kwenye Zahanati ya Goba, iliyopo katika Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam," Luoga alifafanua.

Aliongeza kuwa kwa mwaka huu klabu hiyo inatarajia kutumia kiasi kikubwa zaidi cha makusanyo kwa ajili ya kuendelea kuboresha mazingira ya zahanati zilizopo wilayani Ubungo kwa kufanya ukarabati wa wodi za kina mama pamoja na kununua vifaa muhimu vya kuwasaidia mama na mtoto wakati wa kujifungua.

Goba Roads Runners (GRR) ni klabu ya michezo inayotambulika na Shirikisho la Riadha Tanzania (RT) kama waandaaji na washiriki wazuri kwenye mchezo wa riadha nchini.

Klabu hii iliyosajiliwa na Baraza la Michezo Tanzania kwa cheti chenye usajili namba 12420, lengo lake kuu ni kuwa jukwaa la kuhamasisha jamii kushiriki mazoezi hasa ya kukiambia kwa ajili ya kupunguza magonjwa nyemelezi yasiyoambukiza, kufahamiana na kufurahi pamoja.

Klabu hii imeundwa na wakimbiaji na wanachama kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, na mikoa mingine ya Tanzania ikiwamo Morogoro, Pwani, Mwanza, Mbeya, Iringa, Singida, Arusha na Tanga.

Kwa mwaka huu GRR inashirikiana na Kampuni ya Jackson GroupSports, ambao watakuwa wanashirikiana kwa karibu kuhakikisha mbio hizo zimefanikiwa vizuri na kutimiza malengo yake.

Akizungumza kwa niaba ya Jackson Group, Levis Paul, ambaye ni Meneja Biashara wa kampuni hiyo, aliwakaribisha wadau wote wa michezo na wengine zikiwamo kampuni mbalimbali, klabu za michezo na makundi ya kijamii kushirikiana na GRR kwenye Goba Hills Marathon 2021 kwa kujisajili na kushiriki kama wakimbiaji au kuwa sehemu ya udhamini wa tukio hilo.




Meneja Masoko wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi (kulia), akimkabidhi mfano wa hundi mshindi wa mchezo wa kubahatisha wa Perfect 12, Samwel Humbe, baada ya kushinda Sh. 145,351,400 na kuwa mshindi wa 94 tangu kuanzishwa kwa mchezo huo, mwaka 2017. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Michezo ya Kubahatisha Mkoa wa Kodi wa Ilala, Shaaban Mwanga. **MPIGAPICHA WETU**

# *Shabiki Yanga ashinda milioni 145/-*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubahatisha ya M-Bet, imezindua kampeni mpya ijulikanayo kwa jina la "Ni Zamu Yako", ambayo imekwenda sambamba na kukabidhi zawadi ya mshindi wa 94 wa Perfect 12, Samwel Humbe, aliyejitambulisha kuwa ni shabiki kindakindaki wa Yanga, wakati akikabidhi hundi ya Sh. 145,351,400 alizojishindia.

Meneja Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi, alisema kampeni hiyo inahamasisha mashabiki wa soka na Watanzania wenye umri kuanzia miaka 18, kuendelea kubashiri na kuwa miongoni mwa washindi ambao watajishindia mamilioni ya fedha kupitia mchezo wa Perfect 12 na michezo mingine ya kubahatisha ya kampuni hiyo.

Mushi alisema mpaka sasa wametumia Sh. bilioni 4.2 kuwazadia washindi mbalimbali kupitia mchezo wa Perfect 12 ambao ulianza rasmi mwaka 2017.

"Humbe ni mshindi wa 94 tangu kuanza kwa mchezo huo wa kubahatisha wa Perfect 12, ambao umeweza kubadili maisha ya Watanzania wengi hapa nchini. Kampeni mpya inahamasisha zaidi mashabiki kuendelea 'kubeti' kupitia M-Bet ambayo kwa sasa imeweza kuwapa maendeleo mashabiki wa soka na kujiunga na nyumba ya mabingwa," alisema Mushi.

Kwa upande wa Humbe, alisema atatumia fedha hizo kuanzisha biashara mpya huku akiwasomesha watoto wake.

Alisema pia ataendeleza kazi yake ya ufundi seremala kwa kununua vifaa vya kisasa na kuifanya kazi yake iwe ya kisasa zaidi.

"Nimefurahi sana kushinda, sikuamini kupata ushindi huu ambao kwa ujumla, naipongeza Kampuni ya M-Bet kwa kuwa wakweli na mshindi anapatikana kwa mujibu wa sheria," alisema Humbe.

Mkuu wa kitengo cha michezo ya kubahatisha mkoa wa kodi wa Ilala, Shaaban Mwanga, alimpongeza Humbe kwa ushindi na kampuni ya M-Bet kwa kutimiza wajibu wake ikiwa ni pamoja na kulipa kodi za serikali.

# Michezo

Jumatano Desemba 2, 2020

Nipashe





Hazard ana wakati mgumu mno - Zidane UKURASA 22

**WAACHENI WAJE...**




Viungo wa Manchester United, kutoka kulia; Bruno Fernandes na Paul Pogba wakifurahia jambo na mshambuliaji wa timu hiyo, Edinson Cavani (kushoto) wakati wa mazoezi ya timu hiyo kuelekea mechi ya Kundi H ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain itakayopigwa Uwanja wa Old Trafford leo usiku. **PICHA: MTANDAO**

# PLATEAU: TUTAPINDUA MEZA KIBABE SIMBA

## Kocha wao asifu soka 'biriani' ila aahidi mauaji kwa Mkapa, kiungo Ndala asema ni zamu yao Dar, lakini...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kupoteza nyumbani kwa bao 1-0 dhidi ya Simba kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Plateau United, Abdul Maikaba, bado ana matumaini vijana wake wanaweza kupindua meza kibabe ugenini, kauli ambayo pia inaungwa mkono na kiungo wa timu hiyo, Isah Ndala, imeripoti BSNSports.com.ng.

Simba ambayo imerejea nchini jana huku ikiahidi kuwashushia wapinzani wao kipigo kitakatifu watakaporudiana Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, iliwashtukiza Wanigeria hao Jumapili kwa kipigo hicho cha bao 1-0 katika mechi iliyopigwa Uwanja wa New Jos, mjini Jos, Nigeria, shukrani zikimwendea Clatous Chama aliyeizamisha Plateau dakika ya 53 baada ya kazi nzuri iliyofanywa na winga Luis Miquissone.

Hata hivyo, Maikaba alikiri kuwa Plateau United haijapata mafanikio kama hayo kabla ya sasa, lakini ana matumaini kuwa yanaweza kutekelezwa na mawazo sahihi.

"Mchezo mzuri dhidi ya Simba SC wanacheza soka la kuvutia ['pira biriani' kama wenyewe wanavyoliita'], lakini si kwamba haishindwi, wapo [umbali wa] inchi chache mbele yetu kwa sababu wamecheza mechi 11 za ligi kabla ya sasa.

> **"Tulifanya hivyo kabla, ninaamini tunaweza kufanya hivyo tena kushinda ugenini mbali na nyumbani. Tunahitaji tu sapoti yenu.**

"Tunahitaji tu sapoti yenu na imani. Bado tunazo dakika zingine 90 kuamua nani anaelekea raundi inayofuata," alisema Maikaba.

Lakini kwa upande wa kiungo mshambuliaji hatari wa timu hiyo, Ndala, amewataka Wanigeria wasipoteze imani kwa sababu bado mbio hazijamalizika.

Ndala ambaye hakufurahishwa na matokeo hayo dhidi ya Simba, aliwaomba radhi mashabiki wa Plateau United kwa kupoteza mchezo huo.

"Hii si jinsi tulivyotazamia mchezo huu uwe, bali kwenye soka ni lazima tukubali kwa matokeo yoyote yanayokuja upande wetu."

Kuhusu Wanigeria kuwatoa Plateau United, Ndala alisema safari ya Dar-es-Salaam itakuwa duwa ngumu lakini Wanigeria hawapaswi kuitoa timu yao kwa sababu bado kuna mchezo wa marudiano.

"Simba imekuja Nigeria na kupata ushindi, pia tutasafiri kwenda Tanzania kuionyesha dunia tunauwezo wa kushinda popote," aliwahakikishia. Akiwa ana hakika kuwa timu yake itashinda jijini Dar-es-Salaam, kiungo huyo alihitimisha na "Msiiweke kando Plateau United."

Plateau United itahitaji ushindi wa mabao 2-0 ama zaidi ili kusonga mbele wakati timu hizo zitakaporudiana Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam majira ya saa 11 jioni, wakati Simba yenyewe itakuwa ikihitaji sare ya aina yoyote au ushindi.

Mshindi wa jumla kati ya Simba na Plateua United, atakutana na Costa do Sol ya Msumbuji ama FC Platinum ya Zimbabwe ambayo katika mechi ya awali nayo ilishinda kwa mabao 2-1 ugenini.

# Azam FC yajipoteza tena kwa Yanga

**Na Adam Fungamwango**

SARE ya bao 1-1 iliyoipata Azam FC kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara dhidi ya Biashara United juzi, Jumatatu, imezidi kuiachia Yanga nafasi ya kuendelea kutamba kileleni kwa wigo mpana wa pointi.

Sare hiyo ambayo ni ya tatu kwa msimu wa tatu mfululizo kwenye uwanja huo dhidi ya Biashara United, inaifanya Azam sasa kufikisha pointi 26, tano nyuma ya Yanga wakati huu timu hizo kila moja ikiwa imeshuka dimbani mara 13, huku Simba iliyopo nyuma kwa michezo miwili, ikiwa na pointi 23 katika nafasi ya tatu.

Azam, ambayo Jumatano iliyopita iliweka rekodi nyingine ya kupoteza mechi kwa mara ya kwanza msimu huu kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Azam Cpmplex dhidi ya Yanga kwa kuchapwa bao 1-0, imekuwa kwenye wakati mgumu kwa siku za karibuni hatua iliyoifanya kumtimua kocha wake mkuu, Mromania Aristica Cioaba.

"Ni kweli hatukupata ushindi kwenye mechi yetu dhidi ya Biashara, hii hatuwezi kumlaumu mtu yeyote kwa sababu ni hali ya kimchezo. Huwezi kusema mbona tumemwondoa kocha na matokeo bado si mazuri. Nikwambie tu mechi yetu na Biashara tukicheza Mara inakuwa ngumu sana. Hatujawahi kuifunga Biashara ikiwa kwao tangu ipande Ligi Kuu tukiwa na makocha wengine huko nyuma, sasa huwezi kusema hawakuwa wazuri," alisema Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia.

Alisema pamoja na kufanya vibaya kwa siku za karibuni, lakini azma yao ya kutwaa ubingwa msimu huu iko palepale, kwani ana imani watafanya vema mechi zinazofuata na kwani ligi ndiyo kwanza ipo mzunguko wa kwanza.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042